Edna Munai: Kama watoto wameshaenda na baba yao, hata waende na mama, sababu hao watoto (**Interjection**)

Com. Ratanya: Na mimi nauliza, kama akikataa, okay, kama huyu baba, ambaye wengi wamempatia watoto wakikataa, ama wakichukuwa watoto, huyu tu atapewa shamba, hiyo ndio ilikuwa swali.

Na ingine ambayo utajibu pamoja, na wale wasichana wengine, ambao waliolewa, watakuwa na haki ya kuridhi chochote kutoka kwa wazazi?

Edna Munai: Hebu rudia.

Com. Ratanya: Ya pili, tuanza na ya pili. Wale wasichana wameolewa, watakuwa na haki ya kuridhi kutoka kwa baba na mama zao?

Edna Munai: Wale wameolewa?

Com. Ratanya: Na wameenda.

Edna Munai: Wameenda? Wapate shamba, hiyo awezi.

Com. Raiji: Okay, asante sana mama kwa hayo maoni yako, jilandikishe hapo. Sasa Jane Wanjala, atafuatwa na Sofia Rajab. Jane Wanjala yuko, mama huyo yuko, karibu mama, Sofia Rajab awe akijitayarisha.

Jane Wanjala: Kwa jina naitwa Jane Wanjala, kutoka Rongai division, Maendeleo ya Wanawake. Mimi nachangia tu moja, kwa sababu memorandum yetu imepeanwa na Councillor Priscilla.

Yangu point moja ambayo ninayo, ni juu ya viti katika vyama mbali mbali kwa upande wa akina mama.

Tungependa akina mama nasi, tupewe nafasi ya kutosha, kwa vyama. Ikiwa ni chama cha K.A.N.U, chama chochote, au kamati yoyote, akina mama wapewe first priority. Hata hao wawe viongozi, wawe wenye viti, ndio wazee wetu, nao tuwe tumetoshana.

Upande wa Maendeleo ya Wanawake, tungependa sisi wenyewe, tuwachiwe kwa uchaguzi. Wazee wetu wasiingilie.

Pia tungependa, mama yeyote akichaguliwa, achaguliwe kutoka grassroot, kuliko kutolewa mama mbali, akuje atusimamie area hiyo, na hata hivyo, akina mama wako wale ambao wamesoma na wanaweza kuendelea hiyo chama cha akina mama.

Pia tungependa kwa nomination, kama ni Councillor, mama pia achaguliwe kutoka uko chini, kulingana na vile mama anajulikana na anaweza kusaidiwa. Kwa hivyo, nomination ya akina mama kwa Councillors, kwa MPs, iwe na kiwango ya kutosha, nasi tuwe na representative mmoja wa akina mama, tukiwa na shida zetu za akina mama, tunamwendea, hili awe akitusikiliza. Asanteni.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mama Jane Wanjala, umesema kuwa mngetaka kitu kimoja, kutokana na censors yenye akina mama walihesabiwa na wakenya wote, akina mama walikuwa zaidi ya nusu ya watu wa Kenya. Hii kiti kimoja, mkipatia, huyu mama ataweza akina mama wenye ni nusu ya wakenya wote.

Jane Wanjala: Kwa sababu mko hapa katiba, tumeweka tu hiyo mtisikilize, na muweke kwa hiyo katiba yenu, hili tuweze kusikizwa.

Com. Raiji: Okay, naona mama Sofia, nafikiri ni wewe umekaribia, asante jilandikishe hapo Jane.

Sofia Rajab: Asante, jina langu ni Sofia Rajab, Makongeni K.A.N.U Maendeleo.

Public finance, biashara ndogo ndogo za akina mama, ambaye wengi wao wanashindwa, hawajiwezi wengine ni vilema, wengine wamefiwa, na wengine hawakujaliwa kuolewa. Ni akina mama wengi wana shida, baisi ningependa, serikali iwapunguzie ushuru wa biashara ndogo.

Kwa akina mama, pia serikali ipange budget, iwakumbuke akina mama katika budget yao. Kusudu hao akina mama ambao wako sokoni, wanauza mboga, wanauza vitunguu, ambayo inawafanya wasaidie watoto nyumbani, waweze kujisaidia.

Ingingine, ningependa serikali au wakuu wa katiba, wafikiri sana juu ya vijana wa kenya, ambao wengi wamesoma na hawana kazi. Vijana wa kike na wakiume. Serikali iwaingize katika jeshi wote, wapewe mafunzo, wapate ujuzi wa kuwatosha. Kazi ikipatikana watafanya, na kama hakuna kazi, wataweza kuulinda nchi yao, na kuwa na uchuzi.

Ya mwisho tu, akina mama katika Rongai, ningependa tu, tupewe haki kabisa, wakati wa uchaguzi. Tusitolewe akina mama viongozi kutoka nje na mbali mbali, tuwachiwe wenyewe kwa sababu akina mama tunafinyika, tunaletewa akina mama kutoka mbali, ambao wana magari makubwa, elimu kubwa, lakini hawaju shida za akina mama huku chini, hawajui sub location iko namna gani, au division. Lakini wakati wa uchaguzi, wanaletwa na wanafika. Kwa hivyo ni hayo na asante.

Com. Raiji: Asante Mama Rajab, jiandikishe hapo. Safina Achor, nafikiri ulizungumza, unataka kuzungumza tena. Okay karibu karibu tu.

Safina Achor: Majina yangu ni Safina Achor, ninaongea kwa upande ya akina mama na upande wa uridhi. Yaani land and property inheritance.

Naongea upande wa uridhi; tunaona upande wa uridhi ni kitu kama shamba, biashara ama pesa ambazo ziko kwa bank. Na wakati mume anapofariki, tunakuta kwamba sisi akina mama, tunakuzwa na shida nyingi sana. Kwa sababu unakuta familia ya bwana, wanakuja pale, mwingine anasema anataka gari, mwingine anasema anataka shamba, lakini ilhali wanasahau kwamba kuna watoto ambao mume aliwacha.

So ningependa, kama ingewezekana, at least sisi akina mama, turidhi mali ya waume wetu. Kama ni title deed ya shamba, iandikwe kwa jina lako.

Na kitu kingine ni kwamba, tafadhali sana wazee, mnajua kuna msemu huwa inasema, mtegemea cha nduguye ufa masikini. So, mtu ajaribu kutafuta chake, atangenezee familia yake akiwa hai. Ni hayo tu sina mengi.

Com. Salome Muigai: Tumesikia malalamishi mengi sana kuhusu shida zenye zinawakuta wajane, eti bwana akisha kufa. Unaona tunaweza kufanya nini kwa katiba hili kuangalia mbele, kuonekana kuwa, kitu gani kina baba wanaweza kufanya wakati huu kuwalinda watu wao kama bado wangali wako hai. Kwani kila mara tunasema wajane walindwe, lakini kitu gani inaweza kufanyika wakati huu, hili hata baba, ama mama pia akiondoka, yule mwenye kubaki, asiwe na hizi shida.

Safina Achor: Kwa upande wangu, ningependelea, mume akiwa hai, aandike kitu ambayo tunaita Will ikiwezekana. Yaani asema nitakapokufa...., lakini hatusemi tunataka akufe ndio turidhi mali. Yaani nitakapo kufa, nafikiria kitu changu, inastahili fulani airidhi, nafikiri ni hivyo.

Com. Raiji: Kabla hatujarudi kwa akina baba, tutamwita mama mwingine mmoja, Mary Cheptoo, karibu mama. Na tafadhali nyinyi akina baba, tuwe kimya tusikilize sauti ya akina mama, hata yenu itasikika.

Mary Cheptoo: Mimi naitwa Mary Cheptoo, nikiwa mama wa Maendeleo na chama cha K.A.N.U, nikawa mimi nimekuja na machangie yetu ya maendeleo ya location, na nitaongea yangu Kwanza.

Ninasema kwa maoni yangu. Ikiwa atachuguliwa raisi katika Kenya, yule anachaguliwa, asisumbuliwe mpaka analize enzi yake. Na kama hana makosa yoyote amefanyia nchi yake, hadumu akiheshimiwa.

Ya kufuata, nchi yetu ya kenya, kila nchi zingine, zisiingilie, kukuja kuchokora, bila matatizo ile anaweza kuchokora nayo. Iwe mwenye kenya, anatatua mambo yao, peke yao, bila kusumbuliwa.

Ingingine, (**Interjection**)

Com. Raiji: I am sorry kuna makelele sana, na unajua hii yote inaingia kwa tape, hatutaki wakati tunarudi tukiangalia tape yaani tunoana kwamba kuna makelele sana, tafadhali tujaribu kuwasikiliza wale wanazungumza.

Mary Cheptoo: Haya, ingine maoni yangu, kama sisi wakenya, tuna shida nyingi kwa manyumba zetu. Tunataka kuingiza sheria yetu, hii sheria hii mpya, kama sisi tumetumia ya wabeberu, ama tulikuwa tunatoa katiba kwa njia ile haikufaa, tunataka nyinyi tume, chukueni maoni yetu, kwa lengo ya kutosha. Sisi wakenya wengine, iliposemekana ati mashamba ya wengine ni kubwa, na wengine hawana, tunataka hivi; mtu ule ananunua shamba lake kwa jasho lakei, awezi kunyanganywa, kwa maana hatujui pesa ile alinunu nayo, si hivyo.

Basi, yakufutwa, kama iko mtu ananunua dunia mzima, hata serikali iangalie, angalau, wengine wapape acre mbili, apate acre tano, na atoe pesa yake kidogo, serikali inaweza kuwa masikini, ipewe loan, halafu itatwanga pole pole, mpaka ajipatie shamba.

Haya yafuata, wale watoto wetu, wamesomeshwa, akisoma, akijipatia kazi ya serikali, asirudi kutatiza wazazi, ama sio mzazi, mzazi fulani amesaidia tu. Mwisho wake, anarudi kutaka kuuwa, apate hiyo shamba, ya hiyo mzazi, na pengine hapana mzazi wake, anataka kuridhi hiyo mbali kwa kibavu, bila huruma yoyote. Hiyo iangaliwe sana na serikali. kwa maana iko mambo kama hiyo. Wengine wanajikimbiza mbele, haende kuchukuwa tite mbele, ile ya haramu, akufuata taratibu, ile jina iko ndani ya register ya shamba ya mwenyew. Hiyo nimesema hayo.

Na elimu ya kimsingi inatakiwa isaidiwe wananchi, mpaka ifikie hata ya secondary, akifika hata hiyo secondary, ang'ang'aniwe na mzazi, na serikali ingaliange wale jamii wako chini sana, kwa shida.

Basi, hii nasema, hiyo mambo yetu chukueni, nyinyi watu wa serikali wanaju a mashamba ile kubwa kubwa kuliko ingine, nataka kuangaliwa. Kama ni ingine inachukuwa dunia mzima, igawiwe wananchi, na anunue.

Com. Raiji: Asante sana mama, jandikishe huko. Sasa tumerudi kwa akina baba (**Interjection**)

Mary Cheptoo: Bado, iko memorandum nataka Priscila asome, ile tumeleta kwa location yetu ya akina mama, asome.

Com. Raiji: Nafikiri ililetwa.

Mary Cheptoo: Hiyo inatoka pande ingine, wacha asome.

Com. Raiji: You brought another memorandum?

Mrs. Priscilla Rono: For a division, this one is a locational one.

Com. Raiji: Okay, ni sawa tu mama, atasoma.

Mrs. Priscilla Rono: Asante, nitasoma kwa haraka.

Upande wa kilimo (**Interjection**)

Com. Raiji: Sema jina lako Kwanza, kwa sababu sasa hiyo ni ingine.

Mrs. Priscilla Rono: Jina langu ni Mrs. Priscilla Rono, Councillor Rongai Ward.

Nitaanza na kilimo; serikali isimamie bei ya kilimo, kama maziwa, mahindi na nyama.

Serikali ichuwe mamlaka ya kiwanda kama KFA, Cereals, AFC, na Kenya Meat Commission, na iendeleze shughuli zao kama zamani.

Siasa; tupewe mamlaka ya kuchaguwa Mbunge, kama hatutosheki na kazi yake, tusingojee miaka tano ikwishe. Kama watu wanaona kiongozi wao ni mzuri, akae kwa kiti mpaka yeye mwenyewe akipenda kustaafu kama raisi.

Mamlaka ya Chief iwe kama zamani, isipunguzwe mamlaka yake.

Matibabu; ugonjwa wa T.B unatibiwa na serikali bure, hata ugonjwa wa sukari na high blood pressure, imemaliza wakenya wengi. Kwa sababu ya gharama. Tungependekeza serikali, iwahudumie watu, bila malipo.

Tabia kwa jamii; ndoa tatu kwa serikali inajulikana, customary. Kanisa na serikali na kwa hizi, ndoa tatu. Mbili inapeanwa cheti cha ndoa, lakini ya kienyeji, haipeanwi. Tungependekeza serikali ipeane cheti yote tatu, kwa ajili inasumbua wananchi.

Elimu; serikali ikipitisha kuwa elimu ni ya bure, iwe bure bila masharti. Na ahadi yetu ya Kwanza, tulipopata uhuru tulisema, tutaondoa ujinga, na sasa bila elimu kuwa bure, hatutamaliza ujinga. Kwa ajili wengi wa watu hawa, hawataweza kulipa karo.

Uridhi; uridhi kwa akina mama kutoka kwa wazee wao, ihimizwe zaidi kwa ndoa. Sheria iwekwe kwamba, mmoja wao akifa, bwana au bibi mmoja wao awe msimamizi wa mali yao. Jamii isingilie mambo yao.

Siasa; nchi nyingi isiingilie mambo ya kenya. Wakenya wenyewe watatue mambo yao. Asante.

Com. Raiji: Asante sana Cllr. Priscilla. Kwanza, nafikiri sasa tutamwita Mheshimwa, ambye hata yeye ni mkaaji wa hapa, aseme au afanye mapendekezo ambaye angetaka, Mheshimiwa karibu.

Mheshimw Erick Murogo: Asante sana. Kwanza ningependa kusema sittoa maoni saa hizi, bali ni shukrani kwa commissioners. Hata, hatujazoe tukiongea, tukisimama.

Basi, commission, ikiongozwa na commissioners wetu watatu, ma afisa wao, wananchi wenzangu, Kwanza ningependa kusema vile tulivyo na furaha kuwakaribisha. La pili, noana.... My name is Eric Murogo, MP Rongai, thank you.

Nimeona vile flow inaenda, singependa hata kusumbua tena, ningetaka hiyo tempo iendelee mpaka mwisho. Lakini nilitaka tu kusema shukrani, na nimeridhika kwamba, wananchi wangu wa Rongai, wanatoa maoni yao, bila kushirikishwa. I would like

this to go in record, kwamba we are very happy, with the way mumehandle tangu asubuhi, mpaka wakati huu. Basi, nitatoa maoni yangu, baadaye. Na nina hakika yale tumesema, naona inaenda kwa record, na nitahakikisha kwamba, yale tumesema, mumeweka, na nafikiri mtaturudishia tuone yameenda namna gani. Mpaka kwa sasa, nashukuru sana. Kile tu nitasema, msikubali sisi wanasiasa, kuwasukuma sana, mpaka mnatoa reporti mbovu kwa sababu wanasiasa wengine wanataka kutoa wale wako ndani. Na wale wako ndani, wanataka kujiendeleza. Chukuweni nafasi yenu, mtupatie kitu ya haki, kitu ambacho kitatujenda kenya hii kwa miaka hamsini ingine. Mungu awabariki sana.

Asante sana Hon. Erci Murogo, MP wa Rongai, ambapo tuko leo. Tunataka kuwahakikishia Mheshimiwa kwamba, kulingana na sheria, tutatengeneza reports kwa constituencies, na tukimaliza zitarudi hapa, hili mwone kama maoni yenu kweli ilifika huko.

Com. Raiji: Kwa hivyo sasa tutaenda kwa Wesley King'ok, Wesly, ni wewe, sema jina ambayo utafuatwa na Shem Busenei.

Wesley King'ok: Naitwa Wesley King'ok, na natoa memorandum yangu, ambayo tumeandika na mmoja wa wananchi wa Kambiamoto, anaitwa Joshua Macharia.

Kwanza nitasoma;

The first thing is that, the sitting president should be open to impeachment, while he (?).

That vice president should be elected by the people.

That president, MPs and Councillors should have a limited term of two terms of five years each. But incase that person proves to be efficient, he can still contest for a third term.

That heads of parastatals public institution should be appointed by independent body, but not the president.

That, Attorney General and Chief Justice, should be appointed by a panel of judges.

That any Bill passed by parliament, must not await the assent of the president, but instead, a jurist of judges, should certify the Bill passed by parliament, with a two third majority.

That Provincial Administration, should be scrapped.

Public servants misusing their positions, and mismanaging the resources of the country, should be prosecuted. And if found guilty, their property be confiscated by the state, and banned from public office.

Politicians, must not hold a public office, that is, while still being a politician, we should not be given an office.

That parliamentary session should be a full time responsibility, and independent tribunal should be set up to oversee the salaries for MPs.

That the constitution should provide for a chance in which the civil society, that is churches, NGOs, should be guaranteed to participate, in case of the constitutional crisis, or issues of national concern.

That a council of elders should be legitimized in the constitution, in order to assist the public in village matters disputes. That is to replace the Chiefs.

Death penalty should be removed completely.

Nominated MPs and Councillor should be scrapped.

Council chairmen and mayors should be elected by the people.

That a country's currency, should not bear the mark of the president. But instead the currency, should bear and identity of national unity or a national monument.

The law should be that, one man one job.

People should have the right to recall their MPs. Procedures should be to solicit for votes of no confidence from the electorate, through a minimum number of vote casted.

That law society of Kenya, (LSK) and the judiciary, should be mandated by the constitution to appoint the electoral commissioners for one term only.

That every citizen who owns a land, should be given a free hold title deed.

Constitution should protect security, healthcare, water, education, shelter, food and employment, as basic rights for all Kenyans.

Constitution should provide a (?) and free primary education.

Men and women should have equal access to land and property right.

That a coalition government should be provided in the constitution.

The constitution booklet should be available at all libraries and public institutions.

That is my last memorandum, but I would like touch on few things that are not there.

That freedom of the press should be entrenched in the constitution. I mean, people should not suppress the press. When people are giving information, we have a society to be informed and it should not be cartelled.

The other thing is; people with junks of lands, with employed inside there, they should ensure that those people get basic facilities like education, and even health services.

Taxation should have a limit, Kenyans are not to be taxed highly, and they should not be taxed just because government wants revenue. We should have a limit of taxation, at a given time. And people should not be compelled to carry their IDs everywhere they go.

And also, the issue of passports, Kenyans should have a right to own passports wherever they want. Thank you so much.

Com. Raiji: Asante sana Wesley, jiandikishe huko. Shem Busenei, ambaye atafuatwa na Sammy Karenjo.

Shem Busenei: Sir, my names are Shem Busenei, I am a retired educational officers, and I come from this area.

I will just be able to give my views on five areas, of which I will Enlight. This is preamble, constitutional supremacy, structures and systems of the government, land and property rights, management and juice of national resources, and basic needs.

So maybe to begin with, I feel and I give my views that, our constitution should have a preamble. To be a vision to our nation, and also to give us obligation to feel that, we have a duty, to participate in the nationalhood. We being one nation, irrespective of our ethnic background, should uphold unity and nationalhood.

The other thing on the preamble is, to guide and to let us know that where the duty, to guard our nationality.

Now, I would like to say something on constitution supremacy. I feel the powers given to parliament, they should retain the power of 65%, but they should also have a commission to vet their decision making.

And I feel also, I feel our MPs should declare their wealth to avoid a suspicion of grabbing the public resources.

Now, the other thing is on structure and the systems of the government. I feel we should have an alternative on types of govern this time. We have been having a unitary government, whereby the powers are centralized. And I feel we should have the regional kind of government, whereby we shall try to decentralize the powers. So that we can be able to have the power within us, we can be able to discuss on our issues very closely. Particularly the management of our resources, budgetary of finances, and also maybe the sharing of the national cake.

Lastly on what I would like to say is about education. I feel, our constitution should address the education need very closely. If possible, we have a free education at least in the lower primary. Where so many children really, they have been cut out, because this basic needs.

Our educational system should be very relevant to our economic. That is what I mean, at the end of producing those who are learning, they should be able to have the skill for self dependence.

Lastly on retirement; the retired people have been neglected in one way or the other. Our constitution, should take care of this group because, after retirement, they should be given care 1, particularly the payment of their benefits.

Sir, I think maybe that is what I had, but in details I have in may paper, thank you.

Thank you very much Bw. Busenei, asante sana, jandikishe hapo. Sammy Karenjo, nilikuwa nimemwita, yuko? Okay, utafuatwa na Philip Bosire.

Sammy Karenjo: Kwa majina ni Sammy Karenjo, kutoka hapa Rongai, Bisei sub location.

Yangu nitatoa report ya kuhusu mashamba. There should be no squatters in kenya.

Land must be distributed and shared equally.

Land sincerely to be 50 acres per person.

Water; the government must give water to all Kenyans.

Reduce presidential powers.

Disabilities; people who are not employed to be given allowance of 5,000 per person.

Inheritance; a widow to inherit husband's property.

Local areas tax to be reduced in license. Nimefika mwisho.

Com. Raiji: Okay asante sana, Bw. Karenjo, tafadhali jilandikishe. Philip Bosire, to be followed by Jacob Chesang'. Wewe ni Bw. Bosire, karibu.

Philip Bosire: Asante, mimi ni Philip Bosire, nimetoka upande wa Kambiamoto.

Maoni yangu juu ya katiba;

Ningetaka kuzingatia upande wa haki za mazingira. Maoni yangu ya Kwanza, namaanisha hivi. Hakuna mwenye ako na haki, kama binadamu ambaye anaishi, aswa wakenya. Ninastaajabu kuona, kuna mahali kuna hii game reserve, wanyama unatapata ma tumbili, nyani, wanaishi acre kama elfu hamsini. Na hakuna resource inapatikana pale, na watu kabisa, mkenya haswa mwenye anaweza lima, anaweza utilize hiyo shamba, wanakaa kwa slum. Hapo unaona mkenya haswa, afanye nini? Hatutumii ile rasilmali ya hiyo shamba. Na hatuna kiwango cha kuweka, hati hiyo shamba, kama kuna shamba fulani, at least watakuwa na mavuno kiasi fulani. Hatuna mpaka wa sheria inasema, kama uko na acre moja, hii acre moja utoe mavuno kiasi fulani kusaidia nchi. Hakina kitu inatuelezea hapo. (**Interjection**)

Com. Raiji: Unapendekeza nini?

Philip Bosire: Napendekeza, shamba kubwa, shamba kama National Park, to be minimized and Game Reserve to be abolished. And to be given to landless people.

Pendekezo la pili, ni juu ya elimu; elimu, watoto wengi wanawacha shule kwa sababu ya kukosa pesa, na kutopata mwelekeo mzuri. Kwa mfano, unapata mtu anasomea kuanzia form four, anasomea maybe Geography, Maths, anapopata college, anapata ya teaching. Na hiyo akusomea pale. Ningependekeza shule iwe kama polytechnic. Mtu asome kitu ili anajua kabisa, mwanzo mpaka mwisho, asije akasomea hesabu, halafu afanye vitu ingine tofauti.

Kama ni tailoring, tailoring mpaka mwisho. Awe kama mtaalamu kwa kitu fulani.

Mengine ni juu ya, maoni yangu ni juu ya uteuzi wa commission. Uteuzi wa commission, sioni haja ya raisi kuingilia vitu kama hizo, kuna ma judicial, hizo ndio ingekuwa kazi yao. Kuna commission ambazo zimeteuliwa, zimekwama, kwa mfano kama hii ya ma devil worshippers. Iiteuliwa kitambo, ikakamilisha kazi, lakini matangazo yake hayakuonekana, yaliishia pale pale tu. Sasa hatuna mahali pa kutete, tujue hii mambo ilienda wapi, na hakuna mwenye atauliza. Mwenye aliteuwa, ndio anaye, na ako na

ukweli, lakini hatuna nini (**Intejerction**)

Com. Raiji: Unapendendekeza nini?

Commission iteuliwe na ma judicials, wateuwe commission. Kama kuna mahali imetokea kosa, na hiyo kwa sheria hakuna, commission iteuliwe ya kutatua hayo maneno.

Ningependa kuchangia pia juu ya wasichana ambao wanapata watoto. Kam msichana amepata mtoto, anajua mwenye mtoto, wa share the same problem na mwenye amempea mtoto, kwa sababu kuna njia nyingi ya kuthibitisha mtoto ni wa nani. Isiwachiwe mzigo kwa msichana peke yake.

Na hali ya msicha kupewa mali, aridhi kutoka kwa baba yake, sioni haja. Sioni haja ati waridhi. Maoni yangu ni hayo.

Com. Raiji: Okay, asante hatuna maswali Philip. Jacob Chesang' nilikuwa nimemwita yuko karibu, karibu Jacob. Tafadhali naona makelele yameanza tena, tafadhali tusikize. Kazi ya leo ni ya masikio tu sio ya mdomo, isipokuwa tu ya mtu mmoja, ambaye yuko mbele hapa.

Jacob Chesang': My name is Jacob Chesang; I come from Kambiamoto.

First and foremost, our constitution should be an expression of hope for all citizens. There should be trust between the ruled and the rulers.

It should describe the degree and the extend of human rule, and the limits of power.

There should be a protection of fundamental and individual rights, that is, respect of human rights.

Judiciary should be dependent from executive and legislature.

There should be respect of the rule of law.

There should be regular, free, peaceful and fair election.

There should be no bribery in election.

Also, there should be equal playing ground for all candidates.

There should be freedom to join any political party, hence there will be no K.A.N.U zones and opposition zones.

Electoral commissions of Kenya, should be free from the executive and the legislator.

Members of the electoral commission should not be appointed by the president.

There should be a government of national unity.

There should be a fair distribution of power.

Our constitution must distribute power, and the rule should be one man one job.

And employment should go with qualification, there should be no corruption in that field.

Our Chiefs, should stop creating Kangaroo courts and cells in their areas of jurisdiction.

Finally; equal distribution and sharing of national resources and development should be enhanced.

Thank you.

Com. Raiji: Asante sana, jandikishe huko. Francis Kigumo, ambaye atafuatwa na Simon Mwangi Mbugua. Francis Kagumo.

Francis Kagumo: Thank you, my name is Francis Kagumo, I come from Kambiamoto. This are my recommendations.

On agriculture; we all know and agree that farming, that is agriculture, is a backbone of our economy. The rate at which our forests are being depleted and exercise for demarcation is alarming. Such that in future, our country will be a desert with no rains. With foregoing, many farmers do not heed extension officers advice, especially on soil conservation. Even when such work is done in affected farmers, many farmers do not undertake that exercise. And since the extension officer has no powers to prosecute, or he is unable to convince the farmer to do that work. If the farmer decides not to do, (Interjection)

Com. Raiji: Excuse me, excuse me, can you please go a little more slowly, and obviously try to summarise. So that you can read the point.

Francis Kagumo: Okay. If the farmer decides not to do that, that is the end of it. We all know the resort of soil erosion. So, if

the law is changed, in such a way that, the extension officer is empowered to undertake measures in ensuring such farmers do their work. Even be able to prosecute. In such a way, measures to prevent deteriorating of land, will be taken seriously by farmers, upon advice by those extension officers.

On presenting the certification, such measures as mandatory planting of trees, in each individual farms should be made lawful. Such that;

- One, if one piece of land is 3 acres and below, he should at least plant a woodlot of not less than a quarter an acre. Also depending on the advice of the extension officer.
- The second one; if one piece of land is more than 3 acres and not more than 5 acres, a woodlot of not less than 5 acres.
- Number three; a piece of land of 6 acres and not more than 10 acres, a woodlot of not less than 1.5 acres. The size of woodlot should depend on the size of the land. that is, the bigger the land, the bigger the woodlot. It is surprising that, even many large scale farms, have not decided what woodlot.

The presiding should always depend on the advice of extension officer, given at that time.

Number two; the local authority. The local authority should be made more powerful, in such matters pertaining to election of business premises. Depending with the area, population, requirement, et cetera, business premises should be started at designated areas. Currently, they are mushrooming everywhere, obscuring our countryside beauty. The result has its consequences, since the county council is charging levies, but legally no such services as cleaning the environment. Thereby for example, flying polythene or paper bags are a common occurrence everywhere, even within the villages. It is (?) affecting the environment, and especially livestock which roams our village. In this business premises, were designated areas, such services as garbage, litter collections, could have been possible. Since council employees will be there to clean it. Now it is not positive, and were applying for a license, one is charged for this service.

Special committee should be set up at local levels, to vet for such applications.

Environment; our environment, is of paramount importance, it should be maintained, et cetera. Therefore, everybody should be made responsible for its maintenance for our future betterment. It should be made a law for, it is mandatory for anyone to dispose e.g garbage, substances from houses, sewers, refuse, in a manner likely to expose the area into environmental hazard. Even the rural areas, disposal of refuse is done anyhowly, by many community members.

Public officers should be more empowered to undertake legal measures against such person or persons, who do not follow up the laid down regulations.

The next one, such industries which engage in production of packaging materials, especially polythenes, should ensure those materials are recycled after use, by opening up centers, where such materials can be taken care and collected.

But marketing, a law should be enacted, banning brokers operation in marketing places. Where farmers who are producers are taking their merchandise.

On administration; such post as Chief, Assistant Chief and village elders should be left at the hand of the community, who should select the best candidate, among those who applied for the said vacancies.

Also, a special allowance should be there for the elders who are assisting the Chiefs and the Assistant Chiefs.

Cost sharing; cost sharing in public offices should be done away with. Even cost sharing in public universities, should be minimized, such that, parent, guardian, should pay at least a quarter of the fees of the sons and daughters. That is all.

Com. Raiji: Thank you very much, please register. Simon Mwangi Mbugu, Simon utafuatwa na Stanley Kolum, na Peter Ndungu Mbugwa.

Simon Mwangi: Kwa majin yangu ni Simon Mwangi, na msisikize sauti kwa sababu sauti iko chini kidogo, kwa shauri ya homa, asante.

Mimi ni mkaaji wa hapa Rongai, na nataka kuchangia, sehemu ile ambao sisi tunaishi. Ile sehemu tunaishi, ni sehemu ina shida sana, kwa sababu wakulima wengi hawana mashamba ya kulima, kwa sababu mashamba kubwa ni ile iko na wale wakubwa, wale walitangulia.

Sasa, kile kitu ambayo ningeliomba kuchangia kwa hii kamati, ni serikali ile itakuja, ijaribu kutafutia mwananchi, ingalao apate nafasi ya nusu acre, aweze kuishi, hili maisha yake iwe inastahili. Kwa sababu, wengi hawana mahali ya kukaa, ni kama kilio tu. Kulea mtoto, ni kukomboa nyumba, jambo lolote, chakula ile yeye mwenyewe anataka kulisha watoto nayo, ni ya ile ile tu, kuchangiwa. Kwa hivyo naona, kama kunawezekana, kulikuwa na serikali ile ilikuwa inatangulia, ilikuwa ina mashamba ilikuwa inaitwa ya settlement, ilikuwa inapewa watu halafu wanalipa polepole. Hata angalao mtu akipewa acre mbili, au acre tatu, anaweza kulipanga polepole, kutoka kwa serikali. na akishindwa, ni serikali wenyewe ndio watajua jinsi watakavyomfanya.

Ya pili, tuna shida sana ya ma hospitali yetu. Watu wengi hawana uwezo. Watu wengine hata kusikia mtoto wake amekuwa

mgonjwa, anashindwa nitampeleka niende nikalipe na nini. Kwa sababu, kule kuenda kwa daktari, kunatakiwa ulipe kadi, hiyo ni jambo ya Kwanza. Urudi usonge mbele kidogo uambiwe ulipe shindano. Kama ningeliuliza, katika ule utawala ambao unakuja katika hii kamati, serikali ingekuwa na madaktari, na sisi tungeliulizwa wananchi wa kenya, tuchangie, ingalao tutoa kila mtu shilingi kumi kumi, au ishirini ishirini. Iwe ni kama kodi ya hosipitali.

Halafu, dawa ipatikane katika hosipitali. Nayo serikali waweke bidii, wawape madaktari mshahara wa kutosha. Hili madaktari waweze kutuhumia kwa njia ya mapenzi. Hiyo ni ya pili.

Ya tatu, kuna jambo inangaisha watu sana, hii ni security. Unasikia kidogo watu wakiwa dukani kwao, wanaingiliwa na majambazi dakika moja, na wanakwishanyanganywa pesa, na polisi yetu haiko. Sasa watu wanachanganikiwa, ni polisi, au ni waizi. Hiyo ndio kitu ambacho kinasumbua wananchi sana hapa. kwa hivyo, inaonekana tangu mwaka wa sitini ya tatu, polisi walikuwa ni watu hatari sana, na polisi walikuwa wako na nguvu. Kwa sababu polisi, kama wangesikia mahali inaibiwa, polisi walikuwa wanaingia hapo haraka sana. Lakini siku hizi, unaweza kuenda kuita polisi na wenyewe unaona hawako. Kwa hivyo naomba kamati, ile serikali itakuja, askari afutwe, kufanya kazi yake ni kazi gani anafanya.

Kwa upande wa utawala, nafikiri sisi tuko na machief, na machief wetu wanatuendesha vizuri tu, sisi hatujaona ubaya wowote. Na Chief, akiwa atakuwanga anakosea, akikosea, wananchi wenyewe ndio wanafaa kumng'oa katika ile mamlaka. Sio kusema ati labda apigwe akae, labda nini, aaha. Akikosea, anang'olewa mwingine anawekwa. Na akistahili kukaa vizuri basi, hiyo ndio kazi ya Chief. Asanteni.

Com. Raiji: Okay, asante sana Mzee Mbugua, tafadhali jilandikishe hapo. Sorry Mbogo. Stanley Kolum, utafuatwa na Peter Ndung'u Mbugua.

Stanley Kolum: Kwa majina ni Stanley Kipkorir Kolum, natoa pendekezo langu binafsi. Nitaanzia na raisi, raisi awe na uwezo wa kutawala wananchi wake, kamili. Bila mtu wowote kumtusi, wala kumchafulia jina.

Bunge; Bunge, Wabunge wasiwe na uwezo wa kujiongezea mishahara, au marupurupu yao. Wawe wakiuliza wale waliochagua kutuwakilisha Bungeni.

Viwete; Viwete washughulikiwe na serikali, wawe wakilipwa pesa ya matumizi yao.

Wazee; wazee zaidi ya miaka sitini, wawe wakipokea marupurupu, kutoka serikali yetu tukufu.

Mazingira; mnyama wowote ambaye anaishi katika mazingira ya serikali, ienshimiwe, isiwe ya kuzuritishwa, wala kuuwawa ovyo ovyo, kama nyani, punda milia, kifaru, nyati. Mtu akipatikana ametesa wanyama kama hawa, anashtakiwa.

Masquatters; masquatters wote ambao wanaishi mashamba kubwa kubwa, zaidi ya miaka mitatu, wana haki ya kukatia hekari isio chini ya hekari tano.

Elimu; elimu iwe ya bure, kutoka darasa la Kwanza, mpaka kidato cha nne.

Machief; machief ambao wanasiidwa na wazee wa mitaa, wawe wakipewa marupurupu. Asante.

Peter Ndung'u: Majina yangu mimi ni Peter Ndung'u Mbugua, na mimi ni mtu anatoka Lengenet location. Na hasa, kwa vile niliandika hapa, nilisema nimetumwa na wazee, na nitaongea juu ya regulate Kwanza. Na ningetaka commission yetu, ambayo tuko nayo leo, ifikirie mambo ya boundary ya sub location, kwa ajili hapa itawapa jawabu moja ya Rongai, na sijasikia ikitajwa.

Kwa ile Rongai constituency, inaonyesha, Rongai iko na eight locations, ambayo kila location ina sub location mbili. Ya Kwanza ni ya Budo ambaye inarutani na Nyadudo. Rongai location ambayo iko na Rongai sub location. Lengele sub location, na Menengai, related to read Visoi. Waseges location, ni ya Mamiji sub location, Asubukia West. Majitamu ni Majitamu location, na Roasorai. Shawa location ambayo ilitengenezwa juzi, imetana kurekebisha na kuitwa Boror, maana ya jina Boror hatujui, pengine wale wanajua, wanaweza kutusaidia, na hiyo inahusikana na Ngecha. Tuko na Kambiamoto location, ambayo iko na Kambiamoto sub location, na ingine sijui wanaita Menengai House, anything like that.

Kuko na Makongeni location ambayo iko na Ruthaga sub location na Majimingi. Ongata location ambayo ni ya nane, ina Kataro sub locatio na Piave sub location.

Sasa, saga iko hapa (**Interjection**)

Com. Raiji: Mzee tunajaribu kusikiliza ni point gani unajaribu kulenga tafadhali.

Peter Ndung'u: Mimi nataka kulenga, kuonyesha commission itusaidie, karatasi hii nitawacha hapa. Kwa ajili sasa tungetaka, kama kwa hiyo mambo yote tuko, according to the list we have, hiyo Rongai location iko na nine location, including. (**Interjection**)

Nataka autonomous ya Rengenet location. Kwa ajili wazee wangu wameniambia, kama itakuwa chini ya Rongai, e include the Chief office, and ask the government where the vote of the Chief is coming from. So they will close it today, and I shall leave this to you.

Com. Raiji: Hiyo tumesikia.

Peter Ndung'u: Hiyo mmesikia.

Com. Raiji: Okay, ingine?

Peter Ndung'u: Haya asante sana. Sasa, yangu hii, ni point kidogo mimi naenda, sitawachikisha. Mambo ya preamble imeongelewa na watu wote. Lakini kwa constitution yetu, pahali inasema, this is the constitution of the republic of Kenya, it should read, this is the constitution of the people of kenya; 1. Kikuyu na customary law yao, mpaka 42, ndio tuwe catered without ethnicity.

Ya mwisho kabisa, tuna watoto na tumelia hapa mashamba, maquatter, nini nini. Lakini, kama serikali inangojea ufikishe miaka kumi na nane, upewe kipande, na uweze kutoa kodi. Mimi naona, na ndiposa tuko hapa, tuwe stakeholders wa commission na kutengeneza constitution. Kwa ajili nikiwa hapa na stake yoyote, sina nyumba, sina nini, ninakuja kutengeneza katiba gani. Itanihusu na nini na mimi sio stakeholder. Mkileta koti baadaye, isemekane wale walitengeneze hawakuwa Kenyan, nitakuwa wapi, Chief siwatanishataki. Ni kama wale watu waliandika ya Kwanza bila preamble, kwa ajili wakiwako, inastahili washtakiwa, kuandika kitu, ambayo haina wenyewe, ni nani aliandika kusudio lake.

Kwa hivyo ningesema, vijana, msichana ama kijana, iwe ni wajibu wa serikali. (End of tape)

Com. Raiji: Okay, hayo ni maoni yako mzee, lakini hata mtu masikini ni mkenya halisi na anapatiwa ulinzi na katiba, hata kama mtu sio tajiri. Katiba sio ya wale wako na mali peke yao, au wako na nyumba, hata shamba. Hata wale hawana shamba, nyumba, mali, pia ni wananchi wa kenya, na inatakiwa walindwe. Asante, jilandikishe hapo.

Ningeseme, hiyo katiba yenu inasema hivyo, sijui ni kazi ngapi. Wapewe matrimonial home, ndio wawe stakeholders.

Com. Raiji: Asante. S. K. Gitonga, ambaye atafuatwa na Sammy Muturi, Gitonga ni wewe mzee, karibu. Interpreter, Kikuyu interpreter.

S. K. Gitonga: *Ritwa riakwa ni Samuel Kaheni Gitonga*

Translator: Naitwa Samuel Kaheni Gitonga.

S. K. Gitonga: *Na njikaraga kuria Guitagwo Mang'u Enterprises, Menengai*

Translator: Nakaa Mang'u Enterprises, Menengai.

S. K. Gitonga: *Ndi kindu kimwe gwendaga kuga.*

Translator: Ningetaka kusema kitu moja.

S. K. Gitonga: *Gingo ndiri yaruga mutwe.*

Translator: Shingo haijaruka kichwa

S. K. Gitonga: *Gingo ndiri yaruga mutwe.*

Translator: Children respect their parents in the new constitution.

S. K. Gitonga: *na atumia mambe haheo gitiyo ni ciana. Riu niundu wa uguo-ri, ngwenda kuga Gatiba iria iguthondekwo athuri*

Translator: Because they brought them up.

S. K. Gitonga: *Tondu matangireretwo ni andu acio-ri, nu ungigitwika mundu mugima kana athii Parliament.*

Translator: Men and women have done a good job, which has not has made people obsessed, kama ile ya business schemes.

S. K. Gitonga: *Ingenicoka ndore-ri, wira uria urutagwo ni athuri na atumia ni wira mwega. Tondu niguo utumite andu marute njuwa iria ciari mwiri.*

Translator: We respect our parents, the older generation.

S. K. Gitonga: *Na nitwaheire aciari aitu ithui gitio.*

Translator: We demand that respect from our children.

S. K. Gitonga: *Na ithui ni tukuhoya u gitio kiu tuheo.*

Translator: We should respect the existing government and the future one.

S. K. Gitonga: *Riu ni undu wa uguo naithui tutie thirikari, iria ikuo na iria igoka.*

Translator: We should be united.

S. K. Gitonga: *Riu ni undu wa uguo-ri, tugie na kindu gitagwo gukorwo tuhana undu umwe.*

Translator: We should have one common language in kenya, like the English, people speaking English.

S. K. Gitonga: *Tuthondeke ruga iria yagiriire gukorwo Kenya, toria Kingeretha kiaragio Githungu.*

Translator: I recommend that Swahili becomes the national language and everybody speaks that language.

S. K. Gitonga: *Tuthondeke ruga iria yagiriire gukorwo Kenya, toria Kingeretha kiaragio Githungu.*

Translator: That all Kenyan people, should speak in Swahili.

S. K. Gitonga: *No mundu ndakaugage ati kau ni gatura kamuthemba muna, ka muthemba muna. Ruga yothe niituike ni githweri.*

Translator: That one national language, is going to unite all Kenyans.

S. K. Gitonga: *Kiria ngwenda gukiuga ni atiriri, thirikari ni irutite wira ona niguthii u ikirutaga no ningwenda ike oguo niguo gutikoneke mundu ugakorwo ena uru wa kurehe ndeto cia kuhitithania andu.*

Translator: That will enable kenya to sepa on evoice, and we shall have no problem.

S. K. Gitonga: *Tondu twaria na mugambo umwe, na Kenya yarie na mugambo umwe gutiri thina ukagia.*

Translator: That the constituti *No ndakai kwirwo aheo tuhu tondu gutiri kindu gia tuhu.*

on should protect private property, individual property.

S. K. Gitonga: *Na nii ndingitwika mugathiriria wa kuga indo cia mundu atunywo ati inengerwo mundu uria utari.*

Translator: That land should not be free, people should be made to buy land.

S. K. Gitonga: *Nonjugire thirikari irore kuria gutari andu, ikire mundu agure no ndakaheo tuhu.*

Translator: There is nothing free.

S. K. Gitonga: *Ona ahetwo kindu gia tuhu ndangihota gukirora.*

Translator: That you cannot be able to care for free things.

S. K. Gitonga: *Ndikwenda kwaria muno, tondu nu ndure haha njaragia. Ngukinyia hau. Na Ngai amuteithie.*

Translator: Mzee amemaliza, Mungu awasiaidie commissioners.

Com. Raiji: Asante sana mzee. Sammy Muturi, utafuatwa na James Kiragu, na Joseph Gitau.

Sammy Muturi: Basi majina yangu ni Sammy Muturi, mimi ni mwenyeji ama ni mkaazi wa hapa Rongai, na pia niko na jambo moja pengine mimi ningeguzia, ambalo nimejaribu kulitega, lakini watu hawajaweza kuliwazilisha.

Jambo hili ni kwamba, sisi wenyeji wa hapa Rongai, tumekuwa na shida nyingi, haswa katika kazi zetu za border border. Kwa mambo mengi ambayo serikali ama wale ambao wanahusika kama wabunge, MPs, macouncillors. Kuna accountabilities ambazo pengine kuna pesa ambao ameakirka ama amepewa waweze kufanyisha miradi hapa. Kwa kweli jambo hilo aliendelei

hapa kwetu. Kwa hivyo ni maoni yangu na wenzangu hao, kuwe na tume, au kuwe na sheria ambayo itakuwa ikifuata hao watu ambao wanapewa pesa kama zile za serikali, waweze kufuatiliwa, kwa sababu, wakati mtu ako kwa uwongozi, afuatwi, lakini baadaye ndio unasikia sasa. Kama ile kesi ya ule mama ambaye alikuwa ni kwa County Council, ndio sasa anafuatwa, lakini akiwa kwa ofisi afuatwi. Sasa tungeuliza, kwa sababu sisi wana border border tunaumia sana kwa ajili ya barabara, tunasikia kuna pesa ambazo zinapewa DDC na hazifanyi kazi kulingana na vile inastahili. Kwa hivyo ningeomba tume hii ya katiba, ione ya kwamba jambo kama hilo, linafuatiliwa. Pia upande wa security, hiyo tunashukuru upande wa polisi, maana sisi wana border border wanatusaidia sana. Maana tunaweza kushirikiana na hao, kwa upande huo. Pia, ningeomba pia, wale wa idara ya Chief, pia hao ningewaomba pia wakati kuna masherehe, hii mambo ya funds, wanachangisha funds, hizo waachane nazo kwa sababu, wakati kama leo tunaona kwa hao watu katiba, hao wenyewe wametoa soda kwa kila mtu. Lakini wale tunapochangisha hizo pesa, tunakuta ni hao ma chiefs, na wale ma officers peke yao wanakunywa. Kwa hivyo jambo hili, liondolewe kabisa.

Nafikiri yangu ni hayo machache, na ningeomba tu, kama groups kama hizo za vijana, kama border borders, tafadhali tujaribu kuonwa, na tuweze kusaidishwa, maana kazi hiyo ni ngumu. Lakini kama tungeweza kuwa na katiba ambayo inatulinda, tuweze kusaidishwa, tunaweza kushukuru na kufurahi, maana kazi hiyo ni ngumu, na kama serikali ama katiba inaweza kutukopesha ma motor bykes, hiyo kazi inaweza kuwa rahisi. Asante.

Com. Raiji: Asante sana Bw. Muturi, James Kiragu you are next, akifuatwa na Joseph Gitau. Okay, James Kiragu you have already presented, so Joseph Gitau, okay you have presented. James Kiragu is not there. Cllr Mary Kamau, hayuko. Martha Kipsang', karibu mama. Atafuatwa na Mutua Joseph.

Martha Kipsang': Kwa majina ni huyu Martha Kipsang, nikiwakilisha akina mama wa maendeleo, Rongai, nikiwa mwenye kiti wa division.

Yangu, ningetaka kuchangia, upande ya akina mama zaidi. Mzigo ule mama anakuwa nayo, akiwa ni mama kwa nyumba.

Ninaanzia upande wa mama akiwa mja mzito, mpaka wakati atakapo pata mtoto. Mama amekuwa na kazi nyingi. wakati anapokuwa na mimba, na wakati anapopata mtoto. Ningependa serikali, ipate ukumu wa kusaidia mama wakati huo sababu ya matibabu yake, na hata ya mtoto. Kwa sababu, wakati mtoto atapokuwa mgonjwa, hata kama ni mwezi moja, saa ingine mama hana pesa, kule hospitali atasema toa ya shindano, toa ya kila kitu hata wakati wa clinic. Kwa hivyo ningehimiza, kama serikali ingeweza kusaidia mtoto huyo anapozaliwa, mpaka afikishe hata umri wa mwaka kama tano na kuendelea.

Pia ningeomba, kama ingewezekana, kweli akina mama wana kazi nyingi. Kutoka saa kumi na mbili, hadi saa tano ya usiku. Wakati huu mchana wote, mama anaumia. Akiwa kama yuko nyumbani, kazi yote inategemea. Pia, wakati hata kama ni mama yuko kazini, kule nyumbani inategemea. Ningeomba serikali, iangalie akina mama, iwapatie allowance kidogo ya kujisaidia nayo.

Na ningeomba wazee pia, wakumbuke akina mama, wawafungilie accounts zao, ya kujisaidia, badala ya kuja kila wakati kuomba mzee hata kidogo, ya kusaidia jamii wakati yeye hayuko.

Pia, hii account ya mzee, kungekuwa ingine ya mama na mzee. Sababu, mkiwa joint account, mama ataridhika na mambo kama hayo.

Tukienda upande wa akina mama, wakati mume wake anapofariki, tumeona akina mama wengi wamesumbuka. Kwa kuwa baada ya hiyo unaona, akina mama wengine, sisi tunaita wezi, kwa sababu ni mwizi amejitokeza. Anasema huyu bwana ni wangu. Unaona mzee anakaa karibu wiki mbili wiki watu, kwa kesi. Ningependa serikali isaidie akina mama, ule wa kwanza kuolewa, awe ni mridhi wa kila kitu ya bwana, zaidi. Ikiwa ni pesa, mashamba, na hata magari. Sababu, baada ya hiyo, mama anaangaika sana.

Ningeomba pia, wasiaidiwe akina mama, vikundi, kupewa kama iko pesa, hili wafanye biashara. Ikiwa wakati huu iko kama COMESA, hii COMESA, ina biashara ya vitu hata kuenda nje. Na kama ingewezekana, akina mama wapewe laini kama hiyo, hili waweze kujitegemea. Kwa sababu akina mama wengi wako nyumbani, hawana kazi.

Ningeomba pia, upande wa kule ma reserve, akina mama wanaangaika juu ya maji. Wengi wanasumbuka mchana wote kutafuta maji, na hata masaa nyingi ni ya maji. Serikali ifikirie reserve kwa akina mama kupata maji, bila hata matown iko maji. Pia, ningeomba kwanba, wasichana wetu, wanapoenda kutafuta kazi, wengi wameangaika, wakifika office, na wako na kila kitu, na sababu labda waambiwe watoe kitu kidogo. Ama labda iko mambo ingine tofauti. Tungependa wakati anafanya interview, iwe ni watu wale wanafanya, ni wale watu wanarecognise kama wazee wa heshima. Hili hata wakati mwingi unaona iko kazi, mtoto amepita na ako na certificate ya kutosha, hata vijana wanasema waonge. Na tungependa hiyo kitu ipotee katika nchi yetu.

Pia ningeomba juu ya akina mama, pia natetea akina mama kwa sababu, akina mama wengi wangepata jereha nyingi ya kupigwa. Ningeomba ikiwezekana, kama iko sheria ya kotini ya jamii, mama akikosa ama mtu yeyote akikosa, itatuliwe pale, badala ya kiboko. Badala ya mateke. Akina mama wengi wamepoteza maisha yao, kwa kazi kidogo, ama makosa ikitokea. Kila mtu anafanya makosa, hata baba utafanya makosa, lakini hakuna mtu atachapa wewe. Kwa hivyo ni heri tuelewane. Hakuna mama anapenda kufanya makosa, labda ni bahati mbaya. Kwa hivyo iwe na court ya kusaidia jamii kwa problem ndogo.

Na pia hata wale wasicha wetu wanapopata watoto, wale wamewapatia watoto, hata hao wachukuliwe hatua. Kwa sababu wengi tunataka asaidiwe, lakini tukisema tuwe tukiwapatia mashamba, tuwapatie nini. Na ule aliwapatia mtoto, ako na raha, kwa sababu anaona ule mtoto ni wake, baadaye ataenda kuclaim. Kwa hivyo ichukuliwe hatua kwa wale wanapatia wasichana

hatua.

Pia ningependekeza kwamba, hiko mambo kama hii ya makaa. Kweli ni wengi wanashida ya pesa, na serikali tungependa iweke laini, kama mtu ako na ukweli na shamba yake, na anaweza kuomba DO a permit, afikie Chief, na Chief aone kweli hiyo shamba inawezekana kupata makaa. Wapate permit, ama wawe na kikundi ya kuongea mambo kama hayo, kwa sababu watu wengi kweli, nchi hii hawana pesa. Kwa hivyo wanategea vitu kama hivyo, kama makaa.

Pia ningechangia kuhusu hii ukunywaji. Hiyo ya mwisho ya ukunywaji. Wale serikali waangalie ukunywaji wa umri gani wanafaa kukunywa, halafu ni pombe haina gani, na ipitishwe kwa sheria, ule ameelewe kiasi, apelekwe kotini. Asanteni. Mimi jina ni huyu.

Com. Raiji: Jiandikishe hapo mama, na tumesema asante sana Martha Kipsang'. Mutua Joseph, hayuko. Joshua Chumo Joshua karibu, utafuatwa na Amos Ng'ang'a.

Joshua Chumo: Maoni yangu ni moja tu. Ile maneno nasikia nyingi ni hii maneno yote ya katiba. (**Interjection**)

Com. Raiji: Tafadhali akina baba na akina mama, tafadhali tusikilise, utitaka kuzungumza kidogo, unaweza kuchukuwa break kidogo, uende uko nje, ukimaliza halafu urudi. Hii unaweza kutoka na kurudi, lakini ukiwa ndani hapa, tafadhali utege masikio tusikilize mzee, au mama.

Joshua Chumo: Asante sana. Mimi nitakosa Kiswahili kidogo na mimi nitaongea kidogo. Asante sana kwa maneno yenu yote ya katiba. Nyinyi mlitafuta ukweli, na ukweli yenu ni nyinyi. Hakuna wengine watakuja kuchaguwa ukweli ingine, ni nyinyi.

Kitu kimoja, inasumbua watu wengi, ni mtu anazaa watoto kwa bwana, na kuenda na watoto hapo. Ajambo arudishe watoto wa mwenyewe. Mimi naomba serikali kama hiyo, hata mimi ni moja wa kupeleka kitu kama hiyo. Asante sana.

Nyingine kuongea tena, utaongea tena mara ya pili. Iko kitu kimoja, watu wengine wako na shamba ndogo ndogo, na watu wa Bunge si kuulizana kura, wanakuja wanajazana huku. Siku inaenda, inaenda miaka tano, inaringia, nataka kuja tena, naye naenda kabisa. Hawa wananyanyasa, pesa ya maziwa, hakuna, ile shamba ndogo mahindi hakuna. Naenda cereal, hao wanararua, maziwa wanararua. Sasa, mimi naomba katiba ikuje, hii mpya itakuja, hii katiba mpya kukuja sasa, iweke sisi kuomba, iwekee sisi cereal. Halafu ile mahindi yetu kidogo kidogo ipelekwe huko, na ipeleke sheria ya kutosha, ya katiba. Mtu akifanya makosa, ndani, mtu akifanya makosa ndani. Tena K.C.C iwekwe, serikali hapana kosa chochote, iko na mali ya kutosha. Na hiyo watu wote wanakula elfu mia saba, wanakuja rarua tena sisi manyumbani. Hiyo mimi naomba serikali iangalie watu wengine, isaidiwe.

Pesa ya bursary, kuleta pesa ya bursary ya masikini, ile watu tena wanararua, ile masikini nakaa. Nakaa kabisa ,hao wengine wanaangaika hapa. hata wale wengine hapana kuja kukja hapa saa hii. Hao wameshararua sana, kama hii watu wa siasa ya ukweli. Hiyo ni maoni yangu mimi nasema. Mimi sina maoni nyingi.

Com. Raiji: Asante sana Mzee Chumo, jiandikishe hapo, hata hiyo maoni imetoshwa, asante sana. Amos Ng'ang'a, utafuatwa na Nelson Kibosi, na Sarah Kinyo.

Amos Ng'ang'a: Basi nashukuru kwa jinsi ya kupata nafasi hii. Yangu nawakilisha kanisa la Seventh Day Adventist, katika constituency hii ya Rongai, na nitasema kwa kifupi, maana tumeandika.

Jambo la kwanza, tungetaka kuwe na serikali ambayo ni wacha Mungu. Watu ambao wanaongozwa na Mungu.

Jambo ya pili, tungetaka serikali ambayo ingewa na katiba ambayo itafuatilia amri za Mungu zote, kama jinsi zilivyo. Kwa kifupi, maana ya hayo yote nimeandika mengine, tungetaka tena, sisi kama kanisa la Seventh Day Adventist, ambao ni watunzi wa Sabato. Kama jinsi ambavyo siku zingine, kama Juma pili inavyochukuliwa wakati wa holiday, ikiwa kuna holiday. Kana inalingana na siku ya Juma pili, inasongeshwa mbele. Tungetaka Sabato itambulishwe, maana ndivyo ilivyo katika neno la Mungu. Asante sana.

Com. Raiji: Okay, asante sana Amos. Mwingine ni Nelson Kobosi.

Nelson Kibosi: Jina langu ni Nelson Kibosi, na ninapenda Bwana Yesu. Ninachangia kuhusu jambo machache.

Ya kwanza, kuhusu mambo ya katiba, tunajua kweli ya kwamba sisi tunafundishwa katiba, lakini watu wengi hawajui katiba ni nini. Na ya kwanza, nilisema ya kwamba, tunataka, maoni yangu ni ya kwamba, kila district, iwe district moja, kila mtu achunge mali yake pale. Kwa sababu mtu anaweza toka Nairobi, anaweza toka kila mahali, na anaweza kukuja, mgeni akikuja, wale watu wa hapo hawawezi kuonekana.

Ya pili, ni ya kwamba, kuna mambo mengi katika Kenya yetu, kuna mambo ya uwizi, tunaona kule na kule. Na ningependa ya kwamba, mambo ya uwizi iangaliwe sababu kuiba si vizuri. Na ya kwamba, kuna kazi nyingi katika Kenya, lakini kuna watu ambao wanachukuwa pesa chungu mzima, kwa ajili ya mshahara wao. Hasa, wacha wabunge wetu, nimesikia wakienda parliament, wanababanda mambo ya pesa, iwe nusu million, elfu mia nane, au elfu mia nane, na wananchi wanataabika.

Kuna hata watu hawawezi kupata chakuwa ya jioni, hata lunch, mtu anaweza kuenda mpaka anaanguka barabarani. Ningeliza tu, tume hii, ama katiba ambayo inakuja, ili wananchi waone ya kwamba, katiba ama mshahara ya wabunge, watu raia wenyewe, wanaweza kutoa report kusema tunataka Wabunge wetu wapate kiasi fulani, kwa sababu tunaona ya kwamba, hiyo elfu mia nane, elfu mia tano, ingeandika watu vijana wetu, wengi. Na sasa vijana wakikosa kazi, wanasema uwizi, na wizi

inatokana na ulafi. Mtu awezi kuiba kitu kama ako na kazi, hata kama anapata shilingi elfu tatu kwa kila mwezi. Sasa umefuka pale kwa sababu ya kazi hiyo. Lakini, tukiona mtu anatangatanga pale, anachunga kule rafiki yake, akiona ako na pesa karibu mia tano, ananyemelea.

Ingingine, ya kwamba, tena, upande wa walimu. Tunaona ya kwamba, walimu wako na kazi nyingi, lakini tunaonba hata serikali iko sasa, ama ambayo itakuja, waangalie mambo ya walimu. Kwa sababu walimu ni nguzo ya kila kitu. Unaona wale watu wanakuwa ministers, professors, wanatoka kwa mwalimu. Kutoka chini, mpaka nursery, mpaka university, ni mwalimu. Lakini mwisho, tunaona ya kwamba, walimu wanapata mshahara kidogo, na wenyewe ndio wanafanya kazi kubwa.

Basi ingine, ni kuhusu mambo, sisi wengine ni watu wa kanisa, sisi zote. Kuhusu akina mama, tunaona akina mama kweli, hata wakati wa Yesu, tunaona kwamba, kuna jambo ambalo inasema katika Bibilia. Akina mama wawe wako na kazi zao, ambayo wanaweza kufanya kazi zao. Na kuna wanaume wanafanya kazi zao. Watu msichanganye ya kwamba, mwanamke ni sawa na mwanaume, mwanaume ni mwanaume, mwanamke ni mwanamke. Lakini mradi tu washirikiana kwa (?) hili watu waendele. Kwa sababu tukiona kwa bibilia inasema ya kwamba, usivae mavazi ya wengine, na wanawake siku hizi wanaona ya kwamba, wanapuuzua neno la Mungu. Sisi kwanza ni watu wa Mungu, tuangalie kabisa, tuingie kanisani, tufunze watu, tukiwa kwa mapastors, wafunze watu, ile neno la bibilia wanakataa, wamekataa. Akikubali yes, alright, ni sawa.

Basi ingine, ni ya kwamba, asante, ni kuhusu mambo ya magari, ambayo inatembea barabara. Mambo ya accident, kila wakati. Ipunguze speed yake, kwa sababu tunaona ya kwamba, watu wanakimbia mbio, na watu wa matatu hawajali mwanadamu, wanajali pesa. Jambo hilo, ninaona ya kwamba, ndio inaleta hasara katika kenya yetu. Kila wakati nasikia accident, karibu mara nne ama mara kumi kwa siku. Kwa hivyo ni hayo tu, ninasema asante.

Okay, jiandikishe hapo. Sasa baada ya huyu alikuwa ni Mee Nelson Kibosi, nilikuwa nimesema Sarah Kinywa, yuko? Sara? Kama hayuko, nitamwita Cllr. Mary Kamau, nilikuwa nimemwita alafu alikuwa ametoka, lakini amerudi. Na kabla mama hajazungumza iko tangazo fulani. Naona tuko na watu wengi sana hawajapata nafasi, na labda mapendekezo mengi yamesemwa, tungewaomba sasa, kwa sababu hili kila mtu apate nafasi. Labda tupunguze muda kidogo, kutoka dakika tano, hadi tatu, na tujaribu kupendekeza yale ya muhimu, na pengine yale labda hayajaguziwa na wengine. Hili kila mtu akitoka hapa, awe amepata nafasi, hiyo ni sawa? Kwa hivyo tu (Noises) Unajua vile tunataka ni kwamba, mtu akilenga ile pendekezo, kwa sababu ile tunataka ni ile kitu tuweke kwa katiba, lakini unajua wakati mwingi unapotea wakati watu wanatwambia story nyingi ni mzuri na tunaolewa lakini, ile tunataka tu ni ile tutaingisha uko kwa katiba. Kwa hivyo, tutapunguza muda kidogo, hili watu wote wazungumze. Au msemi tupatie mtu moja nafasi azungumze mpaka usiku, turudi, unaona hiyo sio vizuri.

Okay mama sasa, wewe ndio wa mwisho wa dakika tano.

Mary Njoki Kamau: Majina yangu ni Mary Njoki Kamau.

Na pendekezo langu la kwanza, ni ya kwamba, katika katiba, iteuliwe mahakama ya kuwashughulikia watu masikini, ambao wanashindwa kuweka wakili, na badala yake, kunyanganywa mali zao.

La pili, ni elimu ya msingi kuanzia nursery katika Kenya. Iwe ya bure, isimamiwe na serikali, kwa sababu wakenya wengi ni masikini na hata kupeleka watoto nursery, inakuwa vigumu.

La tatu; watoto werevu kutoka jamii masikini, waelimishwe na pesa kutoka katika hazina ya serikali.

La nne; mishahara ya walimu, ambao wanafanya kazi nzito sana katika nchi yetu ya Kenya, haiwezi ikalinganishwa na ingine yeyote. Wapewe mishahara ya kutosha, hawana nafasi ya kuenda kufanya kazi zingine, kwa sababu kazi ya walimu ni mchana na usiku, saa yote, na mambo ya watoto wetu. Mishahara ya walimu iwe zaidi.

Vile vile, macouncillors wapewe mishahara ya kutosha. Kwa sababu hao ndio wana kazi ngumu, kwa sababu hao ndio wanakaa na raia huko vijijini, na kila mwananchi anamtegemea Coucillor, kwa sababu wakati mwingi, wabunge wanakuwa Nairobi.

Na vile vile, mshahar wa Councillor ukishakuongezwa, uwe ukitoka katika hazina ya serikali, hili kupunguzia ma Council shida.

Vile vile, mamlaka ya raisi ipunguzwe.

Na mishahara wa raisi na wa mabunge, upunguzwe.

Vile vile, ma Chief ni wazuri, lakini wawe wakichaguliwa na raia wenyewe, baada ya muda wa miaka mitano.

Utawala wa Wilaya, yaani , P.C, D.C na ma D.O, wanafaa kufutiliwa mbali. Kwa sababu wanatumiwa kuwanyanyasa wanao tetea haki za wanyonge.

Na hili linge, wenye tunzi wa mali ya nchi, na wali pora mali ya taifa hili, iundwe mahakama ya kuwalizimisha warudishe mali waliopora ya wananchi hataka kama ni mashamba, hata kama ni pesa.

Waliopigania uhuru wa nchi hii mababa zetu, walikufa na wakapoteza ndugu zetu, hawajalipwa vidia na serikali, tangu ichukuwe uongozi. Kwa hivyo tunaomba katiba hii, iwalipe watoto wao vidia walio hadhirika wakati wa kupigania uhuru wa nchi hii.

Wahanga wa vita vya kikabila ya 1992 na 97, vile vile, serikali iwalipe vidia.

Vile vile, iwepo sheria ya kuwalinda akina mama, kutokana na dhuluma ya kudharauliwa na kunyanganywa mali zao. Na vile

vile, watoto wasichana, wagawe mali ya wazazi wao, sawa sawa na watoto wa viume. Kwa sababu hata watoto wasichana, tunawaona, ndio wanajali wazazi kuliko wanaume. Kwa hivyo wagawiwe mali ya wazazi wao. Sawa sawa na wanaume.

Lingine; katiba ya sasa, imulinde kila mkenya, popote alipo, pamoja na mali yake. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Mama una dakika nusu ya kumalizia.

Mary Njoki Kamau: Na vile vile, katiba hiyo ya kenya, ambayo inalinda mali na maisha ya wakenya, zaidi iwashughulikie wananchi wanaoishi katiba sehemu za shida, kama vile Turkana na area zingine, wafikiriwe zaidi.

Na katika utawala wa uraisi, au Mbunge; ni vizuri raisi wa nchi hii, awe kiongozi ambaye ana familia. Kwa sababu hata bibilia inasema, kiongozi asiwe bila familia. Tuongozwe na raisi aliye na familia.

Vile vile, tutaiyomba katiba ya wakati huu (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Jambo ya mwisho Mama.

Mary Njoki Kamau: Yes, vile vile, tungeiomba katiba ya wakati huu, ihakikishe kila mkenya ana shamba, angalao hata kama ni kidogo, asipatikane squatter katika Kenya, kwa sababu kuna mashamba makubwa sana, ambayo hayana watu na hali watu wanaridhikana katika mavipanda.

Asante sana Mama Diwana kwa maoni hayo yako mazuri.

Na la mwisho tafadhali, watu wazee kuanzia miaka sitini , watunzwe na hazina kutoka serikalini, kwa sababu tunaona watoto wa siku hizi, hawajali wazee wao waliwazaa. Kwa hivyo, serikali ijenge kiwango cha kuwatunza wazee. Hayo ndio maoni yangu na ya wananchi wangu.

Com. Salome Muigai: Asante sana, tunafurahia hayo maoni yako mazuri. Michael Mwago, Bwana wakili alikubali mfanye kelele kidogo kidogo, mimi ni mwalimu, na mmewatetea sana walimu kwa kazi mzuri yenye tunafanya. Moja yenye tunajua sana ni kuuliza watu wasipige kelele, wakati tuko darasani. Kwa hivyo tafadhali ningewaomba tunyamaze, hili tusikilizane. Hii wakati yenye tunapiga kelele pia inachukuwa muda, na huo ni muda wenye munahitaji kuzungumza. Kwa hivyo tafadhali tungempata Bw. Michael Mwago, yuko? William Kambo, William sasa wakati ni dakika tatu, so you have to be totally totally well prepared.

William Kambo: My names are William Kambo Muchai.

My first opinion is on the electoral system and process. My opinion is that all defectors, they lose their parliamentary position once they defect.

On basic rights; on the clause of human rights' freedom of worship, it should not infringe on other aspects of social justice. Especially when we have public speakers, and they interfere with the harmony and disturbance in the public places.

Then on the issue of trade unions; workers should have the right of representation, and the legal system should protect them and keep their immunity. Whereby they can be affected and abused by their employers.

We have the rights of vulnerable groups that, people with disabilities should be protected by law, to avoid abuse, by either omission or commission. For example, we have public place of worship or social places, there should be facilities that protect the disabled people, especially the pavement, instead of stairs and visual and audio facilities.

Children should be protected from abuse by parents and others, especially where they are denied the right of education.

Women as part of affirmative action, should be given this priority of having the provision of educating people, especially in primary and secondary and tertiary level, on issues of gender parity.

Then land and property rights; it is my opinion that pre independence KNUA treaties and agreements should be revoked. In order to promote national intake on land ownership. And those children should have the right to inherit.

On the issue of agriculture; farmers should be involved in regulating imports and exports, and marketing of farm products, especially when we come to some produce like maize, wheat, sugar and others.

And environment; it is my opinion that, littering, those found littering should be prosecuted in the court of law. Thank you.

Com. Salome Muigai: Thank you very much, have yourself registered, thank you for keeping to your time. Peter Korir. Na Peter atafuatwa na David Kamau, aje karibu, na Peter Theuri.

Peter Korir: Thank you very much. Mine I will start with the government. the government (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Utaanza na kutueleza jina lako.

Peter Korir: Yes, I am Peter Korir.

Government; we should have a president who is a ceremonial president, head of state.

We should also have a prime minister, who is in the head of the government.

The parliamentarians, should be people who have education, and as splited by the current constitution, let all that is there, be taken into consideration, but at least when it comes to constituency levels, let it be on population level, and marginalized areas be given more representation.

Also, when it comes to issues of policing, especially security, we have a lot of interference because, there is a ministry which has been dealt below. We have one to be reinstated the ministry of defence, who will in turn be appointing those who are heading all this police forces, and be approved by parliament. And again be assented to by the prime minister.

When it comes to the issues of human right, I would like to mention the statutory law, mentioning the human right issue to prospect human life. It should state from conseption to death. Meaning, it should do away with the capital punishment.

On the issue of disability, we are actually urging that, it should be entrenched into the constitution that, all constituencies, should have facilities for the disabled people. All constituencies should have facilities for disabled people.

Again now, when it comes to the issues of the representation in the councils. We would like to have within every constituency, they have a council or a town council at least. Or for those who have gone further in development, let us have a Municipal Council. So, in every constituency we must have an urban council or a town council, or a municipal council, depending on its level of development. For example here in Rongai, we don't even have an urban council. We are always subject to Municipal Council or County Ccouncil of Nakuru, and this delays and delays the development. Thank you very much.

Com. Salome Muigai: Thank you very much Mr. Korir, you kept to your time. David Kamau. David atafuatwa na Peter Theuri halafu George Waweru.

David Kamau: Thank you, My name is David Kamau. My contribution.

I want to start with on the preamble. I want to suggest that the preamble in the new constitution, be such that, its ownership will be the people of the republic of Kenya. And that, it will allow the individuals of this country to live anywhere in this country, without any kind of discrimination.

On the constitution itself; incase of amendment, it should not be done like the way it is done today, in the parliament, by 222

people. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Hold the microphone at your mouth, so that you can go on record, we are recording.

David Kamau: I was saying that ,it should not be done by 222 people who are in parliament, as if it is done in the case today. It should be thrown back to a referendum by the public.

And on the commission, that will conduct that referendum, it should be elected by the parliament, and any other stakeholder, be it the law society of kenya, churches, this are the people who should come out with those who sit in the commission of the referendum.

On the legislative; all the appointments of the public institution, should be vetted by the parliament, that is by the sub committees of parliament, relevant to that appointment. For example, if it is an institution to do with telecommunication, it should be subjected to a sub committees, which knows about the telecommunication. And the individuals who preside such institutions should be dedicated enough.

Nominated MPs should only be people who represent interest which were not elected, during the normal election. For this one I want to emphasis that, if we didn't have lawyers within the first election by the voters, then the MP, the nominated MP, should now represent the absence of the lawyers or engineers in that matter.

The executive; the president should be a graduate in future, we are not short of graduates.

Second, he should be a model, a family person who is excelling in his family, we can see it as an example.

And in future, instead of having Kangaroo advisers, who we do not know what they are telling the president, we should have a think tank around the president. And established think tank of people who are achievers by their own virtues.

The president, the future president should not be above the law, can be impeached for breaching the contract, of which the public has given him.

Judiciaryl as the case is today, you can see that so many people have made into judicial position, and yet their education is questionable. I would like to say that in future, the stakeholders, the N.C.K, the Women Lawyers Federation, should all be involved in appointments of future judges and magistrate, into their position.

About land (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Lastly.

David Kamau: Land, I would say that, we change from freehold position, to leasehold. So that we can have proper use of land.

Com. Salome Muigai: Thank you very much for those provisions and observation. And before I hand the mic back to the chairman, I would like to say that the next person is Peter Theuri, to be followed by George Waweru, and then Alice Chelaiche, and Susan Chemweno.

Peter Theuri Ndirangu: My names are Peter Theuri Ndirangu, a technician by profession. I would like the government to provide with trade certificates for every businessman before he gets the licence from the county council so that this will help to eliminate the health and other hazard problems.

The government traffic police should undergo motor vehicle and petrol and diesel engine courses so as they should differentiate a bad vehicle which is supposed to be the main road and the one which is supposed to be out of the road.

Kenya Bureau of Standard is supposed to be at large because everybody who undergoes or think that he is supposed to do or make anything he just make, especially packing milk, packing waters, they just pack provided he got the licence without the Knowledge of the Kenya Bureau of Standard.

Private hospitals should provide with the treatment cards for further examination because in most clinics you just get numbers, you get one, three, twenty, then you just go and sometimes they treat you, some hedex, they get you some piritons and you got malaria. So it can only provide with the cards, its very earsier for another officer, a clinical officer to undergo the examination.

We go to inheritance; every child, either married or not married, she or he is supposed to inherit unless there is a will of the parent. Its only that. Thank you.

Com. Riungu Raiji: George Waweru, George Waweru yuko? Okay tutarukia tutafute akina mama. Alicen Cheraite, Nilikuwa nimemuita Alicen Cheraite, Which group? These are ladies here, Susan and then Anna Irungu, Sofia, these are different groups.

Alicen Cheraite: Here Mr. Chairman we have Bina Achimo, we have Loise, Susan myself and the rest so we are going to referend our recommendations together. Mr Chairman we have two memorandums one on issues affecting women in Rongai constituency and another one is on land issues and issues pertaining property rights of women. Mr. Chairman I'm requesting you give us 10 minutes because we presenting together. Thank you Mr. Chairman.

Mr. Chairman, we are going to start with the issues affecting women. Mr. Chairman on citizenship Mr. Chairman, we as women of Rongai we feel everyone has to have a right to equal protection, freedom from discrimination, freedom from expression and association, the directive principles of equitable representation of both gender.

Equality before the law for all citizens regardless of gender of status should be enshrined in the constitution.

Mr Chairman on citizenship, we feel Mr. Chairman are being disadvantaged and we are asking for persons both at Kenyan citizens, within or outside Kenya, whether the parent is the father or mother should be an automatic citizen of Kenya. Watowo wetu wamepata shida kwa sababu ya wasichana wetu, zinakuwa discriminated, hawakubaliwi kuingia Kenya lakini ya wanaume, wote wanaingia; hata akileta mchichana kutoka nje, anakumbaliwa.

Mr Chairman, we also want to say that on citizenship, when issuing title deeds, watoto wa single mothers, wamekuwa discriminated wakienda kwa chief, wakienda kwa registrar, wanaambiwa walete jina ya baba na mama. Tungeomba tukiwa wamama ya kwamba, mtoto atabuliwe na mzazi yoyote, ikiwa ni baba ama mama. Kwa sababu kama single mother hana bwana, atatabua bwana kutoka wapi? Na umesikia kimbele wanaume walikataa affiliation act ilitupwa. Na tungeomba hata kwa haya iwe reviewed.

Another one is about the passports, ama identification, ipewe kwa wamama bila kupakuwa kusema lazima walete jina ya baba ama ya bwana.

On basic rights and basic needs Mr. Chairman tunajua basic rights and basic needs are also women's rights. Kwa hivyo kile tungetaka kuweka maanane, wakina wamama wanahangaika kwa upande wa chakula. Saa ile iko jaa, wamama ndio wako na shida na tungeomba serikali waweke constitution iwekwe maanane ya kwamba mtu Kenya asikufe kwa sababu ya ukosefu ya chakula. Watoto wengi wamama wengi wametoeka, wamakufa kwa sababu ya kukosa chakula.

Free education kwa watoto wetu kutoka nursery mpaka secondary school na universities ziwe cost sharing.

Squatter, shelter iwekwe maanane pia kwa constitution kwa sababu wenye wako na shida ni wamama na watoto. Wakiwa squatters, wamama ndio wanalala kwa makaratasi na watoto na wanaume wanaenda kutembea, mwenye yuko shida ni mama.

Tukija pia kwa upande wa the rights to all property, tungenema hiyo all Kenyans should be equal irrespective of gender or marital status should be upheld by the constitution.

Affiliation act, ile ilitupwa 1967, iwe entrenched in the constitution irudishwe kwa sababu umesikia ya kwamba watoto wetu wamejaa mitaani ama huko kwa ... wamekuwa mapipa kwa sababu ya kukosa baba. Kwa hivyo hiyo affiliation act mnajua vile inasema irudishwe.

Kwa affirmative action Mr. Chairman, tungependa affirmative action tuensure ya kwamba one third of representatives of opposite gender iwe ni akina mama ama ni wazee, iwe imekuwa entlined in the constitution ili legal requirements hata kwa akina mama, hata social discription or culture asiwe discriminated against women alone. Iwe ni ya Kenya mzima.

Mr. Chairman ingine katika education, tungependa equity in this one kwa sababu ikiwa na opportunities ya kazi tunatka watoto wetu wakiwa vijana, na wasichana wachukuliwe pamoja. Na wasichana wetu wasitumiwe wakienda kuomba kazi, wanaambiwa kwanza mbaki mpaka saa kumi na mbili. Hiyo iwe constitutional issue. Watoto hawa wako katika streets, zimetokeana hata na hiyo opportunitists. Wakienda kuomba kazi wanaambiwa abaki nyuma.

Ingeni Mr. Chairman on political issues, tugesema ya kwamba political parties zote zile ziko na Nition outlook ziwe funded by the government. Isiwe tu ni part moja, sisi akina mama tunasea zote wawe funded kwa sababu hiyo ni pesa ya uma. That is also wawe na membership ya national outlook. Kama party haina makabilas zote kwa Kenya hiyo itolewe an tusiwe na parties nyingi katika Kenya, iwe kama tano, ama nne ama tatu. Hakuna haja wale wengine influence opinion tuko tu peke yake.

Ingeni Mr. Chairman niende haraka ni on electoral Mr. Chairman tuntaka secret ballot. Wakina mama wamepata shida kwa hiyo. Tunataka voting system yote iwe inclined na iwe secret ballot ili mama awe na njia ya kupiga kula bila mwanaume kumkataza kwa sababu hapo tumekosewa sana.

Another one Mr. Chairman, civic parliamentary elections iwe separate from presidential elections. Na ya presidents ifanywe kwa separate day. Hiyo sisi tunaona ili tuweze kuchagua watu wenye wanaweza kutumikia vizuri.

Mr. Chairman tukiendelea kwa haraka haraka usituharakishe sana, ni ya kwamba security katika polling day iwe provided na sheria ya electorate commission na ya police iwe harmonized ili electoral commission wawe na power over police siku ya election because wakina mama tumekuwa violated very much, we have suffered. Tukienda hata kutafuta kura tunaogopa kwa sababu election has been carried out and violence has been eminent all the time.

Pia Mr. Chairman tungetaka electoral court iwe established. Isiwe ni ile court ya kawaida, ili kama kuna petitions iwe na special court. Hata wakina mama sisi tunaweza kwenda huko na tunasikizwa.

Minimum qualifications ya MP na councillor ziwe O' level. Hata ya president iwe O' level na kwendelea mbele, preferably awe ni mtu yuko na degree.

Affirmative action Mr. Chairman tunasema hiyo iwekwe kwa constitution mpaka Kenya ifike kiwango ile wamama na mababa wamewai kusaidiana kwa kazi ya kiserikali, kazi yeyote na pia representation in parliament and civic education.

Mayors and chairmen of county councils na ya municipality, na deputies wao wawe elected by the people. Pia president or ministers should not have powers to dissolve councils, hiyo iwe na electoral commission in consultation with the stakeholders,

wananchi wanaweza kudissolve lakini isiwe ni mtu mmoja.

Inginge Mr. Chairman ni ya kwamba the president should not have a constituency. Tungependelea president kwa sababu yeye anafanya kazi ya Kenya mzima, awe president asiwe Member of Parliament. Pia term ya president, tumesema ya kwamba iwe 5 years as it is stated in the constitution na iwe 5 years term lakini akifanya vizuri apewe kuwa term of office and that is full stop.

Na hakuna extension ya parliament. As it is stated in section 59 inasema unless war is prevailing in the country, kama hakuna vita, hakuna haja ya kuextend parliament na hata ile wanasema sasa sisi wamama tunasema hapana.

Interjection

Com. Riungu Raiji: Tafadhali kidogo, ile ya kwanza ya dakika kumi imeisha, nimekuongesha ingine tano, may be you should try uingilie ile memorandum ingine.

Alicen Cheraite: Asante. Constitutional commission Mr. Chairman tunasema ya kwamba a national gender and development commission with at least 50% of women representatives should be established and entrenched in the constitution.

Inginge Mr. Chairman ni a national food commission, sisi wamama tumeangaika kwa hiyo na at least 50% representation be women.

National commission to manage national resources should be established and entrenched in the constitution kwa sababu tukiwa na forest, tukiwa na madini na nini, sisi wamama tukiambiwa tokeni hapo, wamama na watoto ndio wanaangaika.

Constitution Review Commission with at least one third women representation should be entrenched. Hiyo commission yako Mr. Chairman, iwe na wamama one third. Tunashukuru wale wako kwa saa hii.

Local authorities, service commission should be established and ensigned and entrenched in the constitution kwa sababu tunataka macouncillors walipwe na pesa ya serikali kama vile wajumbe wanalipwa. Na tuwe na constitutional commission ama commission ya kuangalia mishahara ya MPs na ya councillors.

Land issue: this is very virtual, tunasema female offsprings regardless of marital status should be entitled to inherit family property. Na majina ya mama na baba iwekwe kwa title deed. Ili baba akikufa mama anasimamia family property kikamilifu. Pia land registry should be decentralized countrywide ili impe wamama access to issue their

Interjection

Com. Riungu Raiji: Just a moment, tafadhali tusipige kelele sana kwa sababu sasa nimemuongesha dakika moja kwa sababu sauti yake ilikuwa imepotea.

Alicen Cheraite: Thank you Mr. Chairman for protecting me. There should be access to land ownership and control of any

other resources among men and women. Sisi zote ni raia ya Kenya. Kenya living in a communal land such as pastoralists should be catered for constitutionally na wawe compensated like any other person. The constitution should be supreme; tunataka constitution iwe supreme to the customary law. Sisi wamama tumeangaika kwa hiyo; iwe supreme, customary iwe chini yake especially concerning land and property inheritance. Title deed ya 99 years hata sisi tukiwa Rongai, matitle deeds yetu ni 99 years. Tunataka iwe freehold ownership kwa kila mtu Kenya mzima ili sisi wenyewe tuko Rongai watoto wetu waweze kuridhi. Title deeds also vile nimesema iwe na majina mawili.

Management of natural resources: tunarecommend ya kwamba, local committees elected by community should manage local resources in their respective environment. Processing industries should be based on the representative areas of production ili employment iweze kupatikana Kenya nzima si pahali pamoja tu kama matowns peke yake.

Defence and national security: Parliament should be given responsibility to national security and be entrenched in the constitution. Constitution should permit the use of extra ordinary powers in emergency situations such as war, national disaster. The minimum number of a parliamentarian for effective emergency powers should be one third. Kenyans who become victims of emergencies or clashes should be compensated properly na wakina mama ndio wako na shida hapo zaidi. Na tena iwe within two years kwa sababu saa zingine wanaambiwa mtakuwa compensated lakini wanakaa hata miaka kumi or forever. Within two years. Local resolution committees with at least 60% of women should be established in security lone zones.

Mr. Chairman ningesema ya kwamba wasichana wetu wapewe property. Tunajua kuna laws inasema ya kwamba wasichana wapewe mali, lakini katika kiutamaduni inapuuza. Iwe constitutionalised na land act yote iwekwe kwa constitution ili isafeguard sisi. Kwa hivyo Mr. Chairman ningetaka kusema ni asante kwa kutupatia 20 minutes. You are kind. Thank you very much.

Com. Riungu Raiji: Asante sana Alicen Cheraite na tume yako, mumejanya kazi mzuri na tutasoma hiyo memorandum tena. Tafadhali tungali tuko upande wa akina mama na tungetaka kumtambua DO wa hapa Irene Odeo. Karibu Mama DO, tumezoea kusema Bwana DO sasa ni mama DO, MP na PDO pamoja na OCS wetu hapa Stephen Mwangi ambaye amekuwa na sisi tangu asubuhi, karibuni. Hii ni kikao cha wazi. Sasa tungali tuko upande wa akina mama, tuko na Susan . (ni yeye mlikuwa naye?) okay. Mama mwingine ni Anna Irungu. Ako hapa? Okay akipata nafasi atakuja. Sofia Langat. Karibu mama. Alikuwa pamoja na hiyo group. Okay karibu karibu. Wapi mtu wa kutafsiri? Hakuna mtu wa kujitokesha hapa? Karibu, Saidia mama tafadhali.

Sofia Langat: *Kainenyun ko Sofia Langat.*

Tlanslator: Kwa majina ni hayo Sofia Langat.

Sofia Langat: *Kainaiyuk kop chon.*

Tlanslator: Nasema majina ni hayo.

Sofia Langat: *Taabu ne kitinye ko lagok che kisiche en gaa amami Kwanda.*

Tlanslator: Shida ilioko ni watoto kuzaliwa nyumbani bila baba.

Sofia Langat: *Amache keger amune sikesiche lagok che ma mi kwanda.*

Tlanslator: Mungalie jambo hilo kwa sababu gani mtoto anazaa bila baba.

Sofia Langat: *Chito ne ndo moet lakwet ko nyalu kotun koik kwandonyin.*

Tlanslator: Yule ambaye anaweka mimba lazima achukue awe bibi yake.

Sofia Langat: *Kosir kebagach lakwanoton koma tinye kiy.*

Tlanslator: Kuliko kuwacha huyo mtoto na huyo msichana ako tu nyumbani bila mali yeyote.

Sofia Langat: *okot ngot ko maitun kemache kosomeshan lakwanoton kot kotar sukul.*

Tlanslator: Na hata akikosa kuchukua afudishe huyo mtoto mpaka analize college.

Sofia Langat: *Ng'alek ab chief konyalu kochaguan bik chief ichegen.*

Tlanslator: Vile vile mambo ya chief, raia watafute chief wenyewe.

Sofia Langat: *Kosir kindewech chief komalewen bik.*

Tlanslator: kuliko awekewe chief na bila vini ya wananchi.

Sofia Langat: *Katen chon.*

Tlanslator: Ni hayo tu

Com. Riungu Raiji: Sasa ni Grace Chebet, Grace Chebet, Grace Chebet yuko? Kama hakuna tunaenda kwa Jane Macharia. Jane Macharia, Karibu.

Jane Macharia: Majina ni Jane Macharia kutoka Rongai. Nikihusia upande wa masingira, Tunajua mazingira ndio huwa inatupatia mvua na hata kujaza manyumba yetu na hata maji. Ningeomba katika hii Katiba tuweze kutengeneza serikali yenye itakuweko iweze kutengeneza mazingira na tuko na watoto wengi wamezurura ovyo ovyo na wanaweza kuwapatia hata kazi waende wapande miti na irudi kama zamani wakati tulikuka ya mbeberu. Itakuwa ni haibu sana tukisema tuko Kenya yetu ni huru na mambo mengi tumekosa kama havo na tunaweza kufanya na mikono yetu.

Ya pili ni kuhusu akina mama. Akina mama wameteseka kwa njia nyingi kama wengine wanafutwa kama kazi na tunajua jukumu kubwa sana ni akina mama katika familia. Mama huwa anafanya kazi mingi katika familia na vile anaweza kuandikiwa barua kama kesho yake anaambiwa hana kazi, hiyo nyumba inaweza firisika. Tunasema kama ni kufutwa kwa kazi kuwe na notice na serikali waweze kuangalia akina mama ndio waweze kuchunga watoto wao.

Ya tatu ni shule, kuhusu shule kutoka nursery mpaka shule ya upili. Malipo imekuwa kali sana mzazi anaweza kugalamia form one na akifika form two anashindwa na kuna hiyo bursary na bursary inaweza kusaidia hao wenye hawajiwezi na watoto ni welevu. Ni hayo tu.

Com. Salome Muigai: Mama asante kwa maoni yako. Tumelezwa na kila mtu mwenye amekuja hapa habari ya kuwapatia watoto wereful bursary. Na masomo ni haki ya kila mtoto, sasa wenye sio welefu ama hatuwaoni kama ni welefu wakatu huo, nao wataenda wapi, kwani kili mtu anamtetea yule mtoto mwelefu?

Jane Macharia: Hiyo nilikuwa ninasema kuhusu kusimamishwa kazi, pengine umetegemewa na jamii, na unaenda huyo mtoto huwa anahangaika hata wewe umesimamishwa kazi na hujalipwa chochote.

Com. Riungu Raiji: Asante jilandikishe. Anna Irungu, Anna Irungu.

Anna Irungu: Nashukuru kwa nafasi hii ambayo nimepewa. Kwa majina ni kama hivyo mimeitwa Anna Irungu, ninatoka Solai na niko na maoni mawili, moja ni vile wanawake wananyimwa nafasi katika kuamua mambo. Kutoka family set up, community set up, hata national level. Tunaona wakati mwingi wanawake hawapatiwi nafasi kutoa uamuzi hata ikiwa ni katika jamaa nyumbani. Tunaona ikiwa mzee anataka kuuza shamba au atake kuuza gari, au msichana wake anaolewa, hata wakati mwingine anaweza kuchukua mahari kivyake, na mtoto aamuliwe ataenda huku. Sasa tumeona, wanawake wanaumia kwa sababu hawapatiwi nafasi ya kuamua mambo ambayo yako katika nyumbani, hata community hata national level. Sasa ni maoni yangu na ningeonelea ya kwamba kama wanawake wangepatiwa nafasi, wawe ni katika familia, mambo ya kifanyika, yawe maoni ya mama yanasikilizwa, anacontribute, na mzee anacontribute sasa wanakuja pamoja ili maoni haya tuwe ni ya kujenga. Pia katika set up, kwa sababu tumejua wanawake hasa ni wengi. Na tunaona hata kwa kuteuliwa katika macommission na mahali pengine popote, wanawake wengi hawapatiwi nafasi. Sasa ni maoni yangu kama wanawake wangepewa nafasi kama vile wako wengi, wasikizwe nyumbani maoni yao, wasikizwe katika community set up hata kwa national level wanawake wanaweza kupeana mambo ambayo ni mazuri na ni ya kujenga.

Kama culture hii yetu ya Rongai, tunaona iko na citizens kama 250,000; nafasi ya hawa, ukichukua kwa population ya wanawake, ni kama 150,000. Sasa tunaona wanawake kila pahali ni wengi lakini maoni yao ya kuamua mambo, hawapatiwi kwa sababu uamuzi unakaa na wanaume.

Oni langu lingine ni wakati wa electoral system being elected in the parliament. Tunaona wakati wa campaign, wanawake

wakijitokeza wafanye campaign ili wachaguliwe katika viti vya ubunge, unaona wanatusiwa sana na wanaume. Wakitusiwa tunaona ya kwamba wanawake ndio wanaogopa. Wanarudi nyuma, tunaona wanawake wanaitwa hata wengine wanaitwa maraya ni wanawake ambao hawana tabia nzuri. Na hapo ndio tunaona wanawake wanarudishwa nyuma sana. Na ndio tunaona hata ikiwa population yao ni nyingi, viti vya uwakilishi na kila pahali wanawake wanakuwa ni wachache kushinda wanaume.

Twanyenyekea tukiuliza hivi, kwa sababu ni kweli wanaume ndio vichwa, na wakiwa vichwa, hatuwezi tukawaruka lakini kile tunaomba ni tupewe nafasi maoni yetu yasikizwe, yawe pamoja na hawa wanaume yakiwa pamoja tuweze kujenga pamoja kutoka nyumbani, community, na national level tujenge pamoja. Asanteni.

Com. Riungu Raiji: Asante sana Anna Irungu, jandikishe hapo, sasa tumerudi kwa main list. Nilikuwa nimemuita George Waweru, amerudi? Kim Francis, Okay ni wewe? Utafuatwa na Richard Korir.

Kim Francis: Asante sana Tume hii ya Katiba, yangu ilie nayazungumzia ni hii: Kuna mambo mingi yamekuwa yakiendelea, jina ni Kimani Francis, na wengi wamezoea kuniita Kim Francis. Ninaongelea maneno kuhusu agricultural sector. Kama mimi mwenyewe ninakuwa mkulima wa kitu kama kahawa, na ni vile nimeshafanya hii kazi, nimefanya kwa muda mrefu, na nitayaona hata wakulima wengi wanakuwa wakiteseka kulingana na vile wanataka haki yao iwe ambao wanatarajia. Mimi yangu ni kusema ni ya kwamba, watu wengi tukiona tunauza ile kahawa tukisiaga tukipeleka kwenye factory, hiyo kitu inachukuliwa na inaenda KPCU na hata wakulima wengine wanalipa kama pyrethrum, wanapeleka mahali wanapeleka, ile pesa wanatarajia kupata, hawapati kulingana na vile ikienda kwa soko yao ile inauzwa, sisi tunapokea kitu kidogo sana na mkulima anateseka kwa sababu anaona hapati haki yake kulingana na vile ilivyo. Kwa hivyo vile ningetaka kusema ni ya kwamba, ningeliza serikali yetu tukufu, hiyo maneno ifuatie maanani ndio wakulima wasifinyiliwe, wawe wanapata vitu vyao kulingana na vile wanataka.

Jambo lingine ni hili, kuna maneno ya hospitali, hospitali unaweza kuona pengine mtu ni mgojwa, anaweza kwenda hospitali, na ni mgojwa sana na hana pesa, akienda kuongea na daktari, kila mahali anaitishwa, nipe kitu kidogo ama hivi hivi, na kwa sababu yeye hana pesa, unaona mtu yule ako na mabilion ya pesa ndio anapokelewa anaenda anaambiwa wewe kuanzia leo, wewe enda nyumbani kwanza, unapewa tudawa kidogo kidogo. Yule ambaye ako na pesa anatibiwa vizuri na yule masikini anaenda tu anaenda kukufia huko nyumbani. Na hiyo tungetaka hata pia serikali yetu tukufu iangalie hiyo maneno vilivyo ndio wale ambao wanafanya hivyo wakomeshe hiyo maneno ya kufinyisha watu sababu masikini na tajiri ni kitu kimoja kwa sababu mwenyezi Mungu wakati alipotuumba, alituumba tukiwa hali moja na hakuna mtu mkumbwa kuliko mwingine isiokuwa tu ni Mungu tu mwenyewe ndio anatumfanya tuwe wakubwa.

Jambo lingine ni la kwamba unaweza kuenda mahali pengine, pengine ni kazi unaenda kuuliza pengine sisi vijana wadogo wadogo mtu anaenda kuuliza kazi pengine ni kuandikwa, unasikia mtu anaitishwa hongo hiyo inaitwa bribes, anaambiwa lete

kitu kidogo nikupatie kazi ama nikuandikishie mahali kazi. Hiyo maneno inakuwa ni maneno ya haibu sana kwa sababu huyu ni mtu anapata mshahara na mimi nimekwenda kuuliza yeye kazi. Tunaona hiyo ni sheria inabidi iingiliwe ndio halafu hawa watu wakionekana na tabia kama hiyo, waeleze vizuri na wadhibiwe kisheria.

Kuna jambo lingine ningetaka kusema, kuna wazee hawa wenye wameretire, National Social Security Fund, unaweza kuona wazee kama hawa, akienda kuitisha ile pesa ya retirement, anaambiwa mzee sasa hakuna kitu, anaendeshwa hivi hivi hivi, hapati haki yake kulingana na vile alikuwa anakatwa pesa. Hiyo serikali tunaomba kwa ukweli ifuatilie haya maanani ndio wazee wawe wanapata haki yao ndio wawe wanafurahia maisha yao mbele ya kukufa.

Jambo lingine ni ya kwamba--

Com. Riungu Raiji: Hiyo ni ya mwisho

Kim Francis: La mwisho ninaona kuna tabia zingine wanawake kuvaa mavasi ambayo haifai kwa nchi ya Kenya. Wanakaa uchi, wengine wanararuliwa maguo town na mahali pengine. Hiyo sheria iwekwe, wanawake wawe wanafaa nguo ile inaofaa kwa sababu ukimwi unaendelea kwa sababu ya maneno hiyo ya usherati. Kwa hivyo mimi ningenelea serikali iweke sheria ambaye mtu yeyote yule, na nikisema hivyo sijasema kwa sababu mimi si Muislam, Waislam wanafanya vizuri wanasema, hiyo ni tabia bovu, na kwa hivyo hata mimi sioni ni vizuri. Ndio tuwe tunaheshimiana, kama mtoto wako akienda uchi na ni mbele ya baba yake na mama yake, haisaidii hata kidogo. Kwa hivyo hiyo ndio nilikuwa tu nasema na ni asante sana macommissioner wetu. Ni hayo tu.

Com. Salome Muigai: Asante sana kwa maoni yako. Mimi nina swali kwako kuwa jukumu la wanaume kwa uwenezaji wa ukimwi, kuna lo ama ni akina mama tu na nguo zao?

Kim Francis: Ni kwa wote.

Com. Riungu Raiji: Asante sana. Richard Korir, Richard Korir? Hayuko. George Gichuki, utafuatwa na Edwin K. Rono.

George Gichuki: Mimi ni George Gichuki kama imesemekana na mambo ambayo nimetumwa na kanisa Katoliki la St. Joseph Lewaka, ni walettee memorandum na nieleze kidogo. Katika mambo ambao wameongea hawa watu wa St. Joseph, wamesema juu ya ukuu wa Katiba ambao wanasema ni kweli katika bunge yetu ya Kenya, chini na tano kwa mia ya vote za wanabunge ndio inapitisha au inaunda Katiba mpya lakini wanasema pengine huwa na ubinafsi, *end of side A* Kuongeza vile wanataka kwa sababu nguvu yote ya sheria iko mikononi mwao. Hapo tungeomba kuwe na makudi mengine ambayo yanasaidiana wakati wanapojadili mambo ambayo yanawahusu kama wabunge, wasiwe na ubinafsi.

Ya pili, ni juu ya vyama vya kisiasa, vyama vya kisiasa hiyo kudi imeonelea zinafaa kuwa chache, si nyingi kama vile tunavyo

hapa kwetu. Ziwe ni kama vyama kumi, ambazo zitategemea vile zimejulikana katika nchi yetu. Pengine chama kikiwa ni cha mtu mmoja ambao kimesajiriwa, hicho si chama ambacho kitatusaidia.

Halafu wakasema juu ya korti zetu za Kenya. Korti zetu za Kenya wanasema iwe independent, isiwe ikiongozwa na state kwa sababu ikiongozwa na state, state ndio mwaajiri, na ndio anaweza sema huyu mtu akiamua hivi, ataondolewa kwa kazi. Yetu ile wameongea.

Interjection

Com. Riungu Raiji: Ya mwisho. Sasa ni moja tu umalize sorry, dakika moja.

George Gichuki: sasa ni juu ya uridhi au vile mtu anaweza kuwa na mali yake. Mali kama sasa mashamba, inafaa kuwa ni mali ya serikali lakini mtu awe anapewa title deed na ikiwa ni mtu ana shamba kubwa sana, ipunguzwe mpaka kama acre mia mbili na hizo zingine ziwe zikitolewa kodi zaidi ndio watu waweze kuhesimiana na kupata mahali pakuishi kila mmoja. Ni hayo tu.

Com. Riungu Raiji: Asante: Tupatie hiyo memorandum. Edwin Kipkirui Rono. Edwin? Hayuko. Richard Chepkwony, Richard na ni wewe, utafuatwa na Christopher Kerich.

Richard Chepkwony: Asante sana kwa majina ni hayo Richard Chepkwony malos. Katika kuchangia kwa siku ya leo, kwa upande wa Katiba, nina maoni moja tu, na ningetaka isikizwe. Ningependa kuona maoni kuhusu wanyama wa poli na binadamu. Maoni yangu ninaona Katiba ilioko sasa hivi, inatamani wanyama kuliko binadamu. Maana kwangu ya kusema hivyo, binadamu akipatikana amefanya makosa, huua mnyama, anachukua _____ kusitakiwa na kufungwa? Na mnyama akiua mtu, binadamu, kuchukuwa siku gapi kutibiwa hiyo kesi yake? Kwa hivyo ningependa kabisa Katiba hili iangalie sawa sawa kabisa kwa sababu katika Katiba ilioko, na ile inakuja sasa hivi mpya, isiwe ya kutishwa na pesa. Kwa sababu kwa matangazo tunayoona, serikali yetu inatamani wanyama wa poli kwa sababu ya kuleta pesa nyingi za kigeni. Mtu akiua mnyama huchukua masaa ishirini na nne, tayari amefikishwa kortini. Na huyo mnyama akiua binadamu, huchukua hata miaka ishirini bila kusikiwa. Gani aliye na mamlaka zaidi? Na vile tulivyo sasa hivi tukiwa watu tunajiweza, tunafanya mambo yetu, tunazungumza, tunaunda Katiba bila kuona mnyama hapa hata moja.

Wabunge kesho wanataka kula kwa wananchi, wananchi hawa ndio watauda serikali wachague wabunge, wachague councillors, na mambo mengine. Hakuna mnyama hata moja. Na hawa Katiba wanasema ya kwamba mnyama huleta pesa nyingi za kigeni, kuna hata mnyama mwingine hajawahi kupigwa picha tangu iundwe hii sirika la wanyama la poli. Na hizo pesa zao huenda wapi? Bona hawalipi _____ wa watu wakati wanaharibu mimea yao? Wakati anapoua mtu, bona hawalipi na wanasema wanaleta pesa nyingi za kigeni? Hizi pesa za kigeni sijui zinaenda wapi. Mimi sina maoni ingine, isipokuwa hiyo tu.

Com. Riungu Raiji: Asante sana kwa hayo maoni mzee. Jiandikishe hapo. Nilikuwa nimesema Christopher Kerich. Ni wewe? Na sasa kwa sababu hatujawapata walemavu wengi, kama wako tafadhali waniambie ili niweze kuwapatia nafasi ndio

waweze kwenda mapema.

Christopher Kerich: Kwa majina mimi naitwa Christopher Kerich, mimi nitaongea kwa upande ya uchaguzi. Kila Mkenya ana haki ya kupiga kura na kusiwe na upendekezo fulani ama chama fulani. Ikiwa ni chama inatawala ama ya upizani, wote wako na haki ya kupiga kura. Nikianza na viti vya madiwani, diwani anafaa kuwa anaelewa kizungu na kiswahili, akiwa na elimu la darasa la nane. Naye nikienda kwa wabunge, mbunge anaweza kuwa mtu wa standard 8 ama wa form 4 ama yule ako na degree. Mishahara yao iwe tofauti kwa sababu kuna maprofessors ambao hawoko kwa bunge na wanapata mshahara dogo na hali yule mbunge wa standard 8 ama wa form 4 anapata nusu million ambayo si vizuri. Nikienda tena kwa upande wa Urais, rais anayeondoka, awe na uridhi, ata akiwa alikosa, asemehewe, na rais yule atakayekuja, asiwe juu ya mamlaka. Sababu ya kusema hivi mtu asiwe above the law, mwanakenya yeyote kutoka kwa rais mpaka raia yule, kila mtu hukosa, na mtu akikosa lazima afikishwe kortini kulingana na kosa lake.

Nikirudi kwa upande ya ardhi, mimi nimependelea mtu awe na acre hamsini. Kwa sababu ya kusema hivi, kuna mashamba ambayo unapata ni acre karibu elfu kumi na ni ya mtu binafsi, na kuna Mkenya ambaye ambaye hata kaburi hana. Mtu akifa anaenda kununuliwa kaburi. Kwa hivyo nafikiri sina mengi kwa hivyo, nilikuwa na mengi lakini mengi yamezungumzwa na watu na sivezi kuyarudia.

Kwa upande wa mshahara ya wabunge, kuwe na kamati fulani, sio wabunge, ya kuongezea hawa mishahara kwa sababu mbunge huyu anakula nono kule na ako na wafanyi kazi kule shambani kwake ama kwake na ananyanyasha hao watu hata pengine hawapei mishahara.

Kwa upande mwingine, ikiwa mbunge akikosa ama Rais akikosa kama hajamaliza miaka mitano, apigiwe ile kura ya kusema no confidence na aondolewe na wananchi. Nafikiri ni hayo tu. Sina mengi.

Com. Riungu Raiji: Mzee Kerich jandikishe hapo, Adrew Rono, Adrew Rono yuko? Inaonekana hayuko. Charles Njenga, Charles Njenga ni nani? Hayuko? Joel Langat, okay utafuatwa na Daniel Juma.

Joel Langat: Mr. Chairman, I want to present a memorandum from the colonel Rongai Branch. So I'm kindly asking you sir if you allow me up to 5 minutes I will clear it. There are two pages only.

Com. Riungu Raiji: You have four minutes.

Joel Langat: Asante. My name is Joel Langat branch chairman, Kanu Rongai branch. Our opinions, feelings, and recommendations for enactment in the new constitution of Kenya, which we believe is people driven. First we would like to take this opportunity to thank most sincerely the President of the republic of Kenya, National Chairman of Kanu, Hon.

Toroitich Arap Moi, present Members of Parliament, Review Commissioners for their total commitment towards the review of the constitution of a unitary government of Kenya which has given us peace love and unity since 1963.

While we appreciate there is need to amend some sections and subsections of our old constitution in line with the swelling growth in population, English demand for food, education, health facilities and other amenities. That does not put off the old constitution in total. Some sections must be retained which will continue to bring Kenyans together.

Our feelings and recommendations should focus mainly on the following area.

That our future president and his Vice President should seek direct votes from the electorate and must garner a minimum of 25% of the votes in at least 6 provinces of the newly proposed 10 provinces of Kenya before we carry out the next general election. They propose two more provinces should be cut from Rift Valley and Eastern Provinces.

That we go to the next general elections with the new constitution in place without compromise. The review commissioners be given enough time they require to give us a golden constitution which Kenyans require.

The post of Prime Minister and its Deputy Prime Minister to be created and the elections through secret ballot by the parliamentarians, both elected and nominated and the contestant must be elected MP and be ready to vacate their parliamentary seats once they are elected to Prime Minister and Deputy Prime Minister for a By-election. Each one of them must garner at least 50% of the votes.

We totally support the creation of at least 90 more constituencies and more so determining factors be geographical, physical, road network, hardship, and not population.

Reviewing of constituencies be done every five years not 10 years, constituencies and civic wards. All natural resources, trustland, forest, wetland be under the total control of the regional government. We are proposing for a regional government especially in every province except Nairobi. Nairobi should remain in the hands of the central government as the symbol of Kenya. Other provincial level to have its own regional government.

Interjection

Com. Riungu Raiji: Last point the time is up.

Joel Langat: The last one is farmers be compelled in the new law to plant 10% of their farms increase to create one forest. Farmers be given prime strategy by central government whenever supplies of commodities drop below the recommended price especially on cereals and _____ or animal products.

The central government to comment in law to buy any substracts cereals store, and market, the same as it is convenient to farmers. Any Kenyan wishing to be elected to lead Kenyans must be literate. Councillors be of at least KCPE or CPE.

Parliamentarian should be of KSCE and above if not trained. Presidential be of a degree holder and of sound mind, healthy, very generous, available 24 hours in naturally parental father and a mother. Sio yule mtu ananunua watoto. Be non alcoholic, a devoted Christian or a muslim, be at least 40 years to 69 years. _____ in our cost is grabbed. In its place we have life imprisonment. Islamic laws be applied in total, we know robbers and thug, Islamic laws be applied as far as ___ and customary marriages is concerned to give room for multi marriages when it comes to inheritance of sharings of property so as to allow 2nd, 3rd, 4th wife to enjoy the same rights as the first wife.

Com. Riungu Raiji: Bwana Langat, that why we have been asking people to summarize because you are reading and we are again going to read.

Joel Langat: Ya, this is the last one. Multipartism: the number of _____ to at least 9 or 5. All high commissioners be compelled in the law to look for job for Kenyans being first, being part of their job. All elected councillors and MPs be covered by a two term rule, that one of President. That is all.

Com. Riungu Raiji: Okay, asante, I think your submissions are clear. You can please give us a copy there. Daniel Juma,

Daniel Juma: Kwa jina ni Daniel Juma kutoka Rongai. Kwanza tunashukuru sana serikali yetu ya Kenya kwa kuwezesha kupatia wananchi kuleta mjadala yao mbele yenu review committee. Tunashukuru sana kwa serikali kuweza kuwapatia wananchi nafasi hiyo kutoa maoni yao bila uoga na bila wasiwasi. Basi kwanza mimi ningependa kutoa mapendekezo yangu juu ya wabunge. Wabunge ambao tunawachagua imekuwa shida sana kwa mwananchi wa Kenya kupata mbunge wake. Mbunge anaenda katika bunge, baada ya kuchaguliwa anamaliza miaka tano, baada ya miaka tano ndio wananchi wanamuona akija kuongea na hawa akitaka kura yao. Basi ningependa sheria itolewe ya kwamba mbunge awe na office katika sehemu ambayo anawakirisha ambaye mwananchi anaweza kumuona wakati wowote ana shida. Kwa sababu huu mbunge anawakirisha mwananchi kwenda kuwakirisha shida zake katika bunge na mbunge ana siku mia tatu ishirini na tano, mara tano, unaona hiyo ni siku gapi ambao anamaliza hizo siku zote hata tukitoka jumapili na siku za holidays bado ana siku nyingi sana na utakuta kwamba siku zake hizo anamalizia huku na baada ya siku hizo kuisha ndio wananchi wanamuona akija kutaka wamuchague tena. Basi sheria hiyo tungependa sana wananchi iwakirishe bungeni ili aweze kuwa akionana na wananchi wakati wananchi wanamhitaji. Sio siku tu ya kutaka kura.

Pia ningependa maoni yangu ya kwamba katika nchi yetu, ukienda katika mijini unakuta watu wengi sana walemavu wameketi kule barabarani wakiomba pesa, shiringi moja, kipofu, kiwete, na serikali imekuwa ikinyamaza kwa muda mrefu sana bila kufikiria hawa walemavu na pia machokora. Serikali iweze kutoa shirika moja ambayo inaweza kuwasimamia hawa walemavu na pia wale watoto machokora ambao wanaleta haibu sana hata pengine ukitembea kule town, unaona anatupia takataka, anakufuata hata na kinyesi, na ni haibu sana. Hata wageni wakitoka kule nchi za ng'ambo wanawapiga picha na kuchukua picha zao na kupeleka kule nchi za ng'ambo na tunaonekana tuko nyuma sana. Ingawa hata nchi hizo ziko lakini tungependa

nchi yetu ionekane ni nchi ambayo tunajiweza na kama vile sisi ni wacha Mungu na Mungu anasema ukisaidia mwenzako nawe utabarikiwa. Ukiona kwamba walemavu wamemalizwa katika njiani kule barabarani na pia wale machokora wamemalizwa katika sehemu hizo za mijini ambao wanasumbua watu sana na kuna uhuru mwananchi akitembea katika mitaa.

Pia hali ya matibabu katika nchini watu wamelia sana kwa sababu serikali ilihudumu cost sharing na cost shairing hii wakati tulikuwa tukinyakuwa uhuru inasemekana ya kwamba, elimu ya bure na matibabu, si bure hivo lakini walituhaidia. Sasa ingekuwa ni cost sharing ambaye mwananchi hata watu wakitembea kule manyumbani utakuta watu wengi sana wamelala wagojwa, hawajiwezi na wengi sana wanaangamia kwa jinsi ya kukosa pesa. Basi tungependa sana serikali itilie maanani sana kwa sababu kama wananchi wa Kenya wote wakikufa bila kupata matibabu, hata ni nani atachagua serikali ya kesho. Kwa hivi waangalie sana hali ya afya katika nchi ya Kenya. Nchi ya Kenya imekuwa na shida sana kwa wananchi kwenda kutibiwa kwa hospitali kwa sababu amekosa pesa na wengi sana wameangamia kwa sababu hata kama ni mjumbe huyo anataka kuchaguliwa, ikiwa watu ishirini watakufa katika area yake, nani atamchagua? Kwa hivyo ni namalizia hapo na nimeshukuru sana.

Com. Riungu Raiji: Asante Bwana Juma. Jiadikishe. Samuel Ruto. Karibu.

Samuel Ruto: Kwa majina ni Samuel Ruto anawakirisha kikudi cha vijana cha double S.

Jambo la kwanza, Preamble: We need a preamble in our constitution to enable the people of Kenya to understand why the constitution is being an access.

Secondly we need the constitution of Kenya once it is ready to be publicized through the press, for example radio.

Structures and systems of government: We propose that we adopt a federal system of government in which the executive and the legislative authority is split between the central government and distinguish regional government.

Land and Property rights: We propose that land be owned individually with a limit in acreage. This limit in acreage should be decided by the regional government of a particular place. The land trities and agreement should be changed according to the peoples demand currently.

Political parties: It is our view that the state and political parties should relate one another with a view to correct the state for the common good of mwananchi. We propose open political parties to allow the tribes to have access to power or leadership in this as this will prevent the large communities from _____ powers.

Defence, national security: It is our view that the parliament should decide future issues of the country for example _____ and emergency powers.

Environment and natural resources. The local community, we propose should benefit from any resources found in their area. The regional government should have the power to enforce laws on protection of the environment and natural resources as per the international set standards. Thank you.

Com. Riungu Rajji: Asante Bwana Ruto. Next is Kenedy Karungu. Ako? Kama hayuko, Joseph Langat, karibu.

Joseph Langat: Kwa majina unasikia naitwa Joseph Langat. Tulikuwa tumetoa yetu lakini sasa hii yangu ni maoni. Yangu ya kwanza ni mambo ya hospitali. Hospitali tumeletewa shida sana kwa wananchi kwa maana unasikia mara wanasema ati hospitali ilipwe pesa. Wakati wanaendelea namna hiyo unasikia tena hospitali imekuwa free. Sasa twataka tujue kwa Katiba hii mpya sasa, wachunguze kabisa vile wanafanya vini ya kusema hii halafu wanasema hii, sasa wananchi wanaweza kuangaika. Leo unaenda unafikiri ni bure, halafu hata kesho unasikia tena imekuwa pesa. Sasa hiyo ni mambo ya upande wa serikali kwa maana hata kama hii wenye private sasa inajulikana kweli unaenda private ndio unajua kweli ni ya pesa. Sasa government anaanza kutoa ___ yao, tena kesho anatoa _____. Sasa napendekeza, aone atoe hiyo malipo iwe free.

Ya pili ni upande wa chiefs na DO. Hawa nafikiri ni mguzo ya wananchi kwa maana kila kitu ikitokea kwanza kabla hajaadikia kwa upande wa police au kuhusu mambo ya mashamba au mambo ya mafurugano hapo nyumbani, kwanza anatangulisha hao machiefs. Sasa nataka kuangaliwe kabisa wapatiwe masupport ya kutosha.

Mambo ya waalimu, walimu wako na shida sana, unasikia saa yote wanasema na wanalia waongezewe mshahara na hakuna mwenye anasikia. Sasa wakati mwingine walilia sana ambayo ikasemekana kweli mishahara itaongezwa, kumbe ilikuwa inasemekana tu ndio hiyo mambo iishe halafu baadaye akatiwe chini, hiyo mambo yao haikutengenezwa vile walikuwa wametangaziwa. Sasa hapo iangaliwe kabisa.

Ya mwisho, upande wa bank, kweli inapeana pesa, loans ya kwenda kusema anataka pesa ya fee inakupatia lakini ile masikini yule mwenye ameenda akapeleka title deed yake huko, anachukua kama elfu mia moja, au elfu hamsini, Sasa wakati atashidwa kulipa, unaona sasa anafanya nini? Hiyo shamba inakuja kuuzwa. Lakini hata angesema hii pesa inatosha kama elfu kumi, ikatwe ile ya kutoshea na pesa yao iuze abakishe zingine. Kwa maana unakuta mtu sasa anatembea barabarani kama shamba imeuzwa yote, na mwenye yuko na pesa mingi kama million tatu, ine, unasikia anatangazwa inasemekana ati huyu amekuwa bankrupt na yuko na shamba na hiyo shamba yake hapana uzwa.

Mwisho sasa ni walimu wa nursery, kweli wanafanya kazi kubwa lakini hakuna wenye wanawashughulikia kulipa hawa mshahara. Sasa mshahara yao ni kutoka mwananchi tena yule, kama hana anakaa bure namna hiyo na kweli serikali ingestahiri ilipe hawa mishahara. Kwa maana si mwalimi kwa mwalimu ni sawa wote? Thank you.

Com. Riungu Raiji: David Kagua, David Kagua, Utafuatwa na Msabo

David Kagua: Mimi jina yangu ni David Kagua Njuguna kutoka Rongai. Maoni yangu ni kama ifuatayo: Kenya should have President, Prime Minister, and both of the places should have Vice Presidencies.

Kenya should have a coalition government. Both the powers of both the Prime Minister and the President should be under the law of the country so that if they make an offence they are directly taken to court like any other citizen.

Parliament should be elected by the public and Kenya should have public service commission which will be responsible for all government servants.

All government heads of ministries, companies and parastatals should be appointed by the public service commission but not the President or the Prime Minister.

Let us come to public public service commission should be elected by the parliament and also the parliament should elect a secretary who will be between public service commission and the parliament. We got to learn every Kenyan citizen, a poor one should have not less than 5 acres of land. A rich person in Kenya with a lot of money and a big land should not have more than 50 acres of land in Kenya. Public utilities, land should not be taken by anybody. Whether the President or Prime Minister.

Hospitals should be free. Many people are dying because of having nobody to pay for the hospital treatment.

Primary schools, and secondary education should be entirely free because poor people in primary and secondary do not go on because of lack of money. University students who are poor should be given full bursaries and with those with money, their payment should be reduced according to the economy of the country. I think those are the good points and (*laughter*) we also have people being trained in various courses

Com. Riungu Raiji: finish point, time is up.

David Kagua: for example teachers joining the parliament, councillors should all have education not less than form four education and councillors and the mayors should all be elected by the public votes. Those are my views and I think you will take them and value them.

Com. Riungu Raiji: Asante, jilandikishe hapo. Mr. Njuguna, tumekubalia hizo points ni mzuri. Musa Abo Karibu Bwana Musa.

Musa Bor: Asante sana mimi ni pastor Musa Bor. Kitu muhimu ambayo mi nachangia ni ufisadi. Neno inasema ufisadi, ufisadi kwa maoni yangu ni mtu ambaye ni muhimu ambaye angependa hii ufisadi ipotee kabisa ni mwalimu. Mwalimu kufundisha kutoka nursery mpaka afike university, kama angepata ya kutosa, hiyo ufisadi haingekuwako. Mtu wa pili ambaye

anaweza kuangamiza ufisadi, ni bwana police, apatiwe mshahara ya kutosha. Hangukuwa na ufisadi katika hii jamhuri yetu ya Kenya.

Schools zote ambayo katika Kenya ni tofauti, iko ____kubwa. Iko mashule ya watu wakubwa kutoka nursery mpaka primary na tunasema tunataka Kenya iwe kitu kimoja. Itakuwa kitu kimoja namna gani? Bila watoto kujurikana wajuane tangu nursery mpaka university. Wananchi wa Kenya hawa hawatasikizana kwa sababu wana tofauti kabisa.

Neno ingine ni squatters, hii neno squatters si mzuri. Kuna mashamba chungu mzima, kuna kazi chungu mzima na mtu mmoja lazima awe na kazi moja. Halafu wananchi wengine wafaidike mtu asiwe anakosa chakula nami nashimba na we bado shimba. Mwizi atakuja, ufisadi itaendelea mbele.

Chief lazima achaguliwe na wananchi na wajuwe huyu ni mtu namna gani anaweza kuzungumza na watu wazuri sawa sawa, si serikali kuandika chief. Chief hachungi serikali anachunga wananchi wale wa chini kabisa .

Bwana commissioner, neno ingine ni bursary. Mnasikia kuna bursary, kuna watoto wa watu wasiojiweza watapatiwa pesa watoto welevu lakini hiyo haitendeki. Bursary hiyo ikitokea lazima watu wale wakubwa wakubwa wale wako na uwezo wanapata hiyo bursary na yule mtu wa kawaida anabaki. Lazima hiyo bursary ipitie kwa subchief, wazee, mpaka nasikia tu hiyo halafu ajue kweli hiyo pesa imeangukia mkono mzuri. Asanteni sana.

Com. Riungu Raiji: Asante sana pastor jandikishe huko. Joseph Ocorner Cheriot, Joseph Cheriot? Mkimuona mtaniambia, John Cherotich?

John Cherotich: Mimi kwa majina naitwa John Cherotich, kutoka Kampi ya Moto. Maoni yangu ni kwamba, tunataka Serikali ya maungano ya Majimbo. Tuwe na Majimbo, ambaye itakuwa na Serikali, yaani Majimbo/coalition government. Kwa sababu, tukikosa kuwa na coalition government, kuna watu wengine hawatawai kuingia kwa Serikali. Kwa hivyo naomba, kwamba tuwe na Majimbo ambayo iko na coalition government.

Neno langu la pili, Bunge, mashirika zote za Serikali, ma-directors wale wanaongoza mambo ya mashirika ya Serikali, wale wanasimamia wawe wakiteuliwa na Bunge. Isiwe mtu binafsi anaamua ni nani anaweza kuongoza shirika ilo. Iwe ni Bunge.

Neno langu la tatu, kuna wakati watu wanaajiriwa kazi, wanasema, uwe Kenyan citizen, na uwe pia na afya nzuri. Je, wale watu hawana afya nzuri, watakaa wapi? Watawekwa wapi katika orodha ya nchi hii? Kwa sababu kila mtu anatakiwa kuajiriwa kazi yeyote, ni yule mtu ako na afya nzuri. So, lazima iwekwe na sheria pia, kwa Katiba ile impya tunatengeneza, hata wale hawajiwezi, lazima wawe na nafasi yao katika nchi hii, kwa sababu Mungu amewaumba hivyo.

Nne, President awe na pia Waziri Mkuu aweko. Tuwe na Waziri Mkuu na manaibu wawili – President na Vice President, tuwe nao. Lakini Serikali lazima iundwe na Waziri Mkuu through Parliament, ili mamlaka igawanywe, isiwe ikikaa kwa ofisi moja vile iko sasa.

Local authorities lazima wapewe nguvu ya kuajiri na kufuta. Isiwe watu wanaenda kwa Minister, halafu pengine hata inaleta shida. Wacha county councils ama tuseme Local Government, local authorities wenyewe waajiri, na wawe na uwezo wa kufuta.

Wazee: tuwe na mahali pa wazee. Mtu akiwa mzee, kuwe na mahali pao pa kulishwa, wakae. Wasiwe watu wa kutupwa, pengine wengine hawana jamii, halafu mtu anakufia kwa verandah ama afe vichorochoroni kwa kurokota takataka akila. Wacha Serikali itenge mahali pa kuweka wazee kama hawa. Zile jamii ambazo zinaweza kulinda wazee wao, yes, lakini kuna wazee wengine ambao hawana jamii. Kwa hivyo, watengewe mahali pao ambapo watakuwa wanakaa.

Mambo ya elimu: kutoka nursery school, kwenda mpaka chuo kikuu, tunaomba Serikali ile inakuja, wacha sasa, kwa Katiba ya sasa, nursery school itambuliwe sana hata kuliko primary school, kwa sababu, yule ndiye msingi. Wacha atambuliwe kwa sababu anafanya kazi nyingi kuliko yule yuko kwa primary school, kwa sababu yeye ndiye msingi, awe analipwa na Serikali. Sio ile inalipwa na wazazi kwa lazima.

Mishahara: tunaambiwa ya kwamba, tunataka watu wafutwe kwa corporations zote. Watu wafutwe kazi, ndio wale wawili wanabaki huko wapewe mishahara kubwa. Hiyo mishahara kubwa, inashtaili watu wote wagawe kidogo kidogo, kila mtu awe kazini, awe akipata kitu.

Mambo ya ukulima pia, sasa ukulima tupewe usito. Serikali awe akitafutia wakulima market, kwa sababu tunaambiwa turudi mashambani. Tunarudi mashambani kutengeneza chakula upeleke wapi? Hiyo ni kilimo, ninaomba hiyo.

Nataka pia kusema mambo ya makanisa. Iwe na mahali pake, iwe na Minister kutoka kwa Serikali ambaye anasimamia makanisa. Makanisa imekuwa kama biashara. Hakuna tofauti kati ya ma-biashara iko dunia hii na kanisa. Kanisa zimekuwa nyingi. Kwa hivyo, kuwe na Minister ambaye atakuwa akisimamia mambo ya makanisa.

Ilikuwa ya mwisho, naunga mkono kwamba, ikiwezekana mambo ya kugawanya wakilishi wa Bunge, igawanywe, nawaunga mkono, hili hata pia watu wengine wapate kazi, sio wachache tu, wawe wakikula hizo pesa Parliament. Asante sana.

Com. Raiji: Serutich. Brother Patrick Kariuki?

Patrick Kariuki: Majina yangu ni Fr. Patrick Kariuki kutoka hapa Rongai. Mambo mengi yamesemwa, lakini, nasema yale ambayo hayasemwa.

Ningeomba ya kwamba, Constitution ya Kenya iko-consider wakati wa reshuffle from one Ministry to the other. They should consider, give humble time for the Minister who has been there, and also to see if the one to be put there is capable. Because, we see that, many funds get lost in- between.

And also, the Permanent Secretaries should not be changed at random. There should be a considere time, to make the..... (inaudible) that they are taken in consideration.

And also, those owning shambas, especially in our country, over 100 acres, they should be charged with high tax so that this goes to help the poor. Wale ambao wako na mashamba makubwa kama acre mia moja, kodi iwe kubwa hili iweze kusaidia wale ambao ni maskini. Na ionekane kwamba kila mwana Kenya ana shamba.

The law should defend the democracy system in the Government, and mostly the Judiciary. Especially, mambo ya ma-korti na kila kitu, lazima kuwe kuna mpango mzuri. Judiciary should be checked so that, especially defending the common man.

The law should favour all people to the last Kenyan, and mostly the weak and the likes of the children.

The Government should ensure the transparency and accountability of the country, and checking all the misuse for the funds, and all the taxes being collected to be used for the common person or the development of the country. Because, if we have a good economy in our country, I think the education and other sectors will improve. We can even have free education, if the economy is well checked.

We should facilitate and promote agriculture and small industries which help the economy of our country, and mostly, reconciliation should be stopped. Hali ya kukatakata miti hapa na pale, kwa sababu, if it affects the sector of agriculture, I think we will suffer a lot in our country. So, that sector should be checked, and also the small industry, like the jua kali which is coming up to support the common mwananchi.

The Constitution should ensure, protect and promote the respect of human rights in all areas, e.g. detention without trial. Mtu akishikwa na kufungwa bila kupelekwa kwa korti, it should be bond, it should not remain the paper, and especially after reviewing the Constitution, it should not remain in the paper. It should be used, especially for the common mwananchi.

More, the Constitution should make sure that there is a free and fair election for all. That is, checking all the rigging, cheating and stealing of the votes. And if something is found that was not right, we should have a by-election.

And more equal rights for women in education and job opportunities. I think many of the other points have been said. Thank

you.

Com. Raiji: Mwingine ni Patrick Muigai or Mungai. Patrick? Mungai hayuko. Amenya Bitmark?. Wewe ni..?

Patrick Muigai: Kwa majina naitwa Patrick Muigai, and I have a few points to make here.

First one is, Constitution should be written in a lay man's language. Hatutaki ikae kama ki-greek, tunataka iandikwe na Kiswahili rahisi na Kizungu rahisi, yenye mtu yeyote anaweza kusoma na kuelewa.

Ya pili, vote of no confidence to non-functioning MPs. Kama kuna Mbunge ambaye tumemchagua, na amekosa kufanya wajibu wake, tunashtaili kumpigia vote of no confidence, atoke, tuchague mtu mwingine ambaye anaweza kututekelezea wajibu wetu.

Ya tatu, copies of the Constitution should be made available in bookshops and bookstands at a very minimal fee or cheap. Tunaomba iwe bei rahisi, ama iweze kupeanwa bure.

And also, we would like the proceedings of the Parliament to be broadcasted live. Iwe broadcasted live, na tuweze kuiona kwa television, tujue vile anasema, kama mtu a-attend ama namna gani.

Ingingine ni foreigners owning businesses here in Kenya. Na ninaongea kuhusu, sijui kama ni vibaya, lakini naongea kuhusu Wahindi. Unapata kuna watu ambao wamechukua biashara hapa na si wa-Kenya. Pesa zenye wanazipata hapa kwetu, wanazipeleka nchi ya nje, wanapeleka marekani na kwingine. Sisi tunabakia na shida hapa na nchi zetu.

Budget should be read at least four months before it is presented to the Parliament or made effective. Tuweze kujua vile Budget inasema kabla kabisa haijaanza kufanya kazi, kwa sababu tunakuta ya kuwa, mambo mengine yanatangazwa wakati wa Budget yanatumiza. For example, the recent increase in kerosene. Kama tungejua mapema, tungenesema isiongezwe kwa sababu mwananchi wa kawaida ndio anatumia.

Title deeds, mimi sikubaliani na wale wanasema ya kuwa, akina mama wawekwe ndani yake. Mimi ningesema ya kuwa, title deeds, tuweke watoto ndani. Kwa sababu, in case of divorce, itakuwa ni problem. Kama bibi anaolewa kesho halafu anatoroka, na ameshawekwa kwa title deed, itakuwa ni problem. So they should be provided maybe with a marriage certificate, in case of any other problem. Lakini, sio kuweka bibi kwa hiyo title deed.

Ya mwisho ni, where do wrong votes come from na kuna watu ambao wana-watch hiyo maneno ya votes. Kwa hivyo tungetaka hizo kura ziwe zikiangaliwa vizuri, na hatutaki kuona kura yeyote ambayo ni mbovu. Nadhania, ni hayo tu niko nayo.

Com. Raiji: Okay, asante Bwana Muigai. Mwingine ni Amenya Bitmark. Utafuatwa na Christine Auguste na John Tisi Matei.

Bitmark Amenya: Asante. Mimi maoni yangu ni machache. Majina ni Amenya Bitmark.

Maoni yangu naonelea ya kwamba, since Kenya is one of the most highly taxed nations in the world, it should provide free primary education for its citizens.

Point yangu ya pili, ninaonelea, because the minimum years to vie for Presidency should be 35 currently, it should be reduced to around 20 years, because we have young people who can be Presidents, who can make it, who can even be better than some old people we have around. So, it should be reduced to around twenty.

Pia, maoni yangu ni kwamba, this capital punishment should be abolished. There is no need of murdering somebody just because he murdered you. Yaani, watu ambao wameua, should be given time for behaviour change – wapate wakati wa kujirekebisha. So, this capital punishment should be abolished.

Pia, jambo lingine ninaonelea ni kwamba, the unemployed people who are above 18, the Government should provide some source of income for them before they get employment. How does the Government expect them to make a living and it is retrenching people? So the Government should be giving some money for the upkeep of these unemployed people, mpaka wapate any sort of employment.

Halafu, maoni yangu mengine ni kwamba, tukiangalia nchi za ngambo, those developed nations. Tunaona, things like rights ya watu kama sex workers, they have been given their rights, it has been legalized. Why can't it be done in Kenya here?

My other view is about abortion. Abortion should also be legalized. We have seen positive effects, we have seen the results in other countries and it has worked there. Why can't we give it a trial here, since, it can also act as a family planning method and other things. Hayo ndio maoni yangu, sina mengi.

Com. Raiji: Okay, hayo ni maoni yako binafsi. Christine Auguste. Wewe ni Christine? Auguste? Huyu ni Christine na ninafikiri ni bibi. Christine, ulijiandikisha kama Christine? Nafikiri iliandikwa vibaya.

Augustine Rono: Kwa majina naitwa Augustine Rono, natoka Lenginet. Memorandum concern in the Constitution making.

Even though Kenya has been independent for 30 years, the citizens have been pressed down for all those years, because, the

Constitution was made in Lanchaster, and it was not fit for a Kenyan citizen.

Citizenship: there should be no condition following anybody born in Kenya as a Kenyan citizen. Born outside Kenya by a Kenyan citizen, should remain a citizen. Required documents as a Kenyan citizen:-

- i. Birth certificate;
- i. National ID card;
- i. Kenyan passport;
- i. Marriage certificate; and
- i. Immigration permit.

Political parties: the Constitution should allow the formation of only two parties.

Structure and system of government: we should retain the Presidential type of government. We should adopt a free, a federation system of government in which the Executive and Legislative authority is free between the Central Government and the distinct regions.

Reason:

- i. For its ruling;
- i. For good security;

Legislature: qualification – at least a good pass at basic education; should have a good communication; a basic understanding of the country, economy and cultural systems.

The people should have a right to recall their MP back home, and immediately elect another one, he or she, when he or she fails to develop his or her constituency. They should act as instructed by their constituents.

The wananchi should determine their salaries. No measures in increasing women participants in Parliament whatsoever.

The President must have powers – he is above the law. The President should have powers to dissolve Parliament because of elections and when there is misunderstanding in the Parliament.

The Executive: the President should be a member of Parliament.

Judiciary: we need a Supreme Court, we need a Constitutional Court. The people should have equal rights, either poor or rich. There should not be a bond in state jailing. Judges must be given transfer after every two years. Any Judge found being

bribed or taking somebody's property has to pay at once and to be jailed. Anybody found as a thief, has to pay back and to be jailed.

Local Government: councillors must be a fourth form or above. Wananchi have rights to recall their councillors and elect another immediately. Wananchi should determine the remuneration of councillors. There should not be nominated councillors.

Com. Raiji: John C. Simatei? John? Hayuko. Karige Kihara? No hapo before, there is Loyce Njenga. Loyce Njenga yuko? Karibu.

Loyce Njenga: Jina langu ni Loyce Njenga, tarafa, kutoka hapa ni Rongai. Mimi ni mjane na mimi nitaongea kwa ajili ya wajane.

Mimi naona, taabu tulio nayo wajane, kwa sababu ukiwajiwa mali, mtoto anataka kuridhi na wewe bado uko hai. Wenye Katiba, chungeni sisi, kwa ajili, hata shamba, hata akiwajiwa kubwa sana, nikitaka kuuza ili nichunge mwili wangu hau niende nayo hospitali, inasemekana, Serikali haiwezi kukubali. Na mimi nilinunua hiyo shamba na bwana yangu. Si shamba ya Kikuyuni, ni ya Rift Valley. Mimi nashindwa ni nini hii, tutakula nini wajane?

Nyumaye, mtoto msichana akiolewa, kijana hataki agawe. Na nilisomesha hao wote pamoja kama ni (inaudible). Kijana ametoka kwangu, akaoa, msichana akatoka kwangu, akaolewa, mimi pekee yangu. Mimi nauliza kwa Katiba, kwa nini hao hapana gawa? Ni mpaka wagawe, kwa sababu wote, hakuna yule ako kwa nyumba yangu, walitoka. Yule alioa na ile pesa alioa nayo, nilipewa kwa msichana, nami nikapeleka kwa kijana. Sasa ni kubadilishana, wote ni wangu.

Lakini mimi naona, watu wa Katiba, tunafinywa sana. Hapa mimi natoka kuna uongo katika Kenya yetu. Kama mimi mzee, kufikiria ni kwa maoni yangu. Unasikia Kenya, mbele, Rais wetu alisema kila mmoja awekewe maji kwake, ili tuwe na uhuru ya maji. Uhuru ya maji tukawekewa, kila mmoja nyumba yetu hapa Rongai, nyingi imesimamishwa mivereji, na hakuna maji. Mimi ujiuliza katika uzee wangu, maji ilienda wapi ile tuliwekewa na kampuni ya maji? Hapo mimi nimetoka.

Watu wa Katiba, mimi naonelea, sisi tunajiua wenyewe na njaa. Kama mtu mmoja alisema, tukaweka msituni, tukaweka nyangau na minyama. Sasa kama sisi tuko karibu na forest, mimi naona sisi hatufaidiki kwa sababu hatulimi. Na moto ilichoma miti ambayo ilikuwako. Sasa hakuna miti ingine, ni (inaudible) tu, na sisi hapana ingia kulima. Sasa mimi naona, hiyo ni kitu moja ngumu sana.

Kwa upande wangu, kama mimi navuna mahindi naweka kwangu, na nyanya, na mboga yangu, nikitokea hapa njiani kuuza, hapo nimeweka meza yangu, council inakuja, inaitisha mimi nauli, mimi nitatoa wapi watu wa Katiba? Na hawa wanaanza kunikimbisha. Nina store, nasimamisha lorry, Mungu alinisaidia mahindi. Sasa mimi nikitaka kupatia hiyo lorry mahindi, watu

wa council wanaingia na kuitisha mimi permit na (inaudible). Mimi nitatoa wapi, na ni kwangu nyumbani?

Mimi najenga barabara kama wengine, sio mimi wengine. Kwenda na barabara, hiyo ni ingine watu wa Katiba. Mimi natoka nyumbani, kama hajafika kwangu, mimi naanguka njiani, sasa kwenda hospitali, hakuna kutibiwa, mpaka nitoe pesa ya (inaudible), pesa ya nini, halafu nitibiwe. Watu wa Katiba, mimi natoa wapi, na mimi nakuwa mwenda wazimu. Hata ile mfuko nilikuwa nayo, ilipotea, mimi sijui iko wapi, damu inatoka, na hakuna mtu wa kunisaidia. Watu wa Katiba, tuna mengi ya kusema. Na, tuseme kweli, katika Kenya. Tukisema sisi tuko na umoja, tuwe na umoja kamili. Tukisema iko ukweli, tuseme ukweli, lakini ukweli hauonekani kabisa kama kwangu mzee, haionekani kwa wenye kutuongoza.

Tukienda ngombe yangu ilichukuliwa, eti ilichukuliwa juzi. Nikienda kwa polisi, kupewa askari kuenda na hawa, tukienda kwa misitu ingine, wanasema sisi hapa hatuwezi kuingia kwa sababu tukiingia hapa, sisi tutakufa. Sasa mimi nitasaidiwa na nani? Tunarudi sisi wote na hawa ndio wako na silaha. Hiyo ndio mimi naonelea, kwa Katiba yangu mzee, hata kama nilikuwa kwa kamati ile ingine. Asanteni sana.

Com. Raiji: Asante mama. Karige Kihara? Hayuko? Joseph Rono?

Joseph Rono: Yangu itakuwa machache, kwa sababu mengi watu wamesema. Yangu tu ni kusema ya kwamba, katika

(Interjection) Com. Raiji: Sema jina.

Joseph Rono: Kwa jina mimi naitwa Joseph Rono. Yangu ni machache, ya kwamba, kulingana na kule kijijini, tuko na watoto mayatima. Na ukiona kabisa, hawawezi kusaidika kwa sababu walipoteza wazazi, hakuna mwenye kufuatilia kuona ya kwamba, nani hasa anasaidia hawa watoto kulingana na shule, kulingana na mahitaji yao. Na tunavyoona ya kwamba, hakuna mwenye kufuatilia hawa watoto juu hawana wazazi, tunashindwa, je, hawa watoto watasaidika kwa njia gani?

Neno lingine, kulingana na kawaida ya raia kuweka Mbunge yao kawaida ya miaka tano, kuna neno lingine ambalo tunaona ya kwamba, ni kawaida Wabunge wakipata hiyo cheo, wao upotea. So, langu ni ya kwamba, mtu akichaguliwa, iwe tena, watu wenye kumchagua, wawe karibu na Mbunge, ili Mbunge asiwe akipotea sana. Wenye kukaa chini na yeye, ajulishwe ya kwamba, kazi hapa ni mbaya, ili tusiwe tukichagua Wabunge kila baada ya miaka tano tunachagua Mbunge mbali mbali, na hawezi kutusaidia, kwa sababu Mbunge yeyote anaingia wakati wowote, anataka kwanza aone kwake. So, langu ni kwamba, tuwe tukiangalia, Mbunge akichaguliwa, iangaliwe kwamba katika positions ama locations, wachaguliwe watu wa kukalishwa chini ya kwamba, sehemu hii ni mbaya, ili aende kwa utaratibu akijua kwamba, sehemu hii inatakikana ifanyiwe nini, na ile nyingine itafanyiwa nini, ili Mbunge asitoroke, ama aone ya kwamba, ako na cheo kuliko wenye kumchagua. Pendekezo langu ni kwamba, tuangalie ilo neno, ili baada ya miaka tunachagua Mbunge tofauti, na sio makosa yake, kwa sababu hakujua ile kazi ambayo amewacha nyuma. Yangu ni hayo, asanteni.

Com. Raiji: Asante sana Bwana Rono. Geoffrey Ndung’u? Utafuatwa na Daniel Kehuga Kimotho.

Geoffrey Ndung’u: Kwa jina ni Geoffrey Ndung’u kutoka hapa Rongai. Basi, nitaendelea kuwasilisha yale niko nayo, hata ingawa mengi yao yamewasilishwa.

Kwa upande wa masingira – yaani forests. Tuko na asili mia tatu ya land cover ya nchi yetu, na ninajua kwa wakati huu, asili mia tatu imegawia ama imekatakata miti ovyo ovyo. Basi ningetaka katika Katiba ya sasa iandikwe kwamba, hiyo sehemu ya forest ambayo ni kidogo sana, ichungwe na Serikali, ama kutolewe sheria kwamba, mtu asikate miti. Na pia kama ni miti ya kujenga, Serikali itengeneze jinsi wananchi wakapopata miti ya kujenga, makaa, na vitu vingine kutoka sehemu hiyo.

Jambo lingine, ni kwa upande wa kilimo. Nchi yetu inategemea kilimo, na unapata ya kwamba, tunavuna mimea na inakosa soko. Na pia, wakulima wakati mwingine wanakosa hata mbegu, ama pesa ya kufanya kazi. Ningeomba katika Katiba ya sasa, policy ya upande wa agriculture, iwe kwamba, wakulima wapewe soft loans, ili waweze kuendeleza kilimo chao na waweze kujajiri.

Halafu, sehemu nyingine ni sehemu ambayo imeguziwa na mwenzangu, ni kuongezea tu. Sehemu hii ambayo, katika Wizara zingine, kuna watu ambao, wengine wameajiriwa permanently na wengine ni temporary. Ningetaka, kwa mfano, waalimu wa nursery school, ningetaka katika hizo Ministries, wale ambao hawaajiriwa permanently, yaani, hawana benefits, waweze kuajiriwa, ili mtu awe na retirement benefits, na vitu vingine ambavyo yule mwenzake anavipata.

Mwisho, ni kwa sehemu ya hawa vijana ambao wanarandaranda katika ma-town zetu. Nimesikia mtu mmoja akiwaita ‘chokora’. Na katika nchi yetu, tuna makabila arobaini na mbili. Kwa hivyo, ningeomba katika Katiba yetu, iandikishwe tuwe na kabila la arobaini na tatu, kwa sababu, kabila ni kwamba, ni watu ambao wanaishi sehemu moja, hawa wanaishi nje, wanakula chakula kile kichafu, hawaribiwi na tumbo, wanaongea lugha yao ambayo sisi wengine wetu hatuielewi. Tukienda iwa ma-towns, tunafunga dirisha. Kwa hivyo, ningeomba katika Katiba yetu, waache kuitwa ‘chokora’, wawe identified kama kabila, na wapewe mahali pa kuishi. Kwa sababu, tumepata mababu...

(Interjection) Com. Raiji: Hiyo tumesikia. Uko na lingine la mwisho?

Geoffrey Ndung’u: Ni hayo tu.

Com. Raiji: Okay. Sasa tunasikia kuna kabila lingine lipya, ni sawa, ni maoni. I think Daniel Kihuga Kamotho? Dakika ni tatu, tafadhali guzia yale ambayo labda hayajasemwa.

Daniel Kamotho: Majina yangu ni Daniel wa-Kamotho, natoka Rongai, upande wa Katitula.

Yangu ambayo nilikuwa nayo, nimeandika, lakini ya kwamba, kitu ambacho nataka kuchangia ni hali ya watoto yatima ambao tuko nao, na ambao wawewacha na wazazi wao wale wamekufa na ugonjwa wa UKIMWI. Watoto hawa kusema kweli, tungetaka Serikali iweke Katiba, ili waweze kutunzwa na kuweza kusaidiwa. Kwa sababu, hawa ndio Serikali ya kesho.

Ya pili, ningetaka kuchukua nafasi ingine tena, kusema ya kwamba, hii hali ya misitu ambayo tunaambiwa, ina forest na ina kila mtu. Kweli, hii misitu, isiingiliwe kwa upande wa kukata miti, kwa sababu kuna askari ambao wameajiriwa katika misitu. Na kuna forests ambao wako uko. Ikionekana makaa, hata tukiwa hapa tunaona moshi ya makaa, na je, askari ambao wako kwa misitu wanafanya kazi gani? Ikiwa mtu yuko nje, anaona moshi ya makaa. Kwa hivyo, hii sheria iendelee mpaka upande ya hawa watu.

Ya tatu, ningetaka kuhimiza habari ya utawala wetu. Katika upande wa utawala wetu, upande wa Rais, ningependa tuwe na Waziri Mkuu ambaye atakuwa akisaidiana na Rais. Na Rais naye, mamlaka ambayo ako nayo, iweze kupunguzwa, ili aweze kufanya kazi na wale wengine. Kwa mfano, watu ambao wanateuliwa kama ma-Katibu Wakuu, wawe wakiteuliwa na Bunge. Watu kama ma-chairman wa ma-kampuni zetu kama parastatals, wachaguliwe katika Bunge, ili, kazi ikiharibika, Bunge ndiyo itaulizwa, kwa sababu hawa ndio waliwachagua.

Nikiendelea tena, ningependa kusema habari ya elimu ya watoto wetu. Elimu, watoto wapewe elimu kutoka darasa la kwanza, hadi form four, ili watoto wote wajue kusoma na kuweza kuandika. Tunakuwa na shida sana katika ma-location, Serikali yetu iendelee katika Katiba, kuona ya kwamba, kila location ina secondary school ya kuweza kusoma na mtoto akirudi nyumbani, kwa sababu wale wanaenda katika masomo ya nje – boarding schools, wawe (inaudible), kwa sababu hakuna wazazi wao. Hiyo ningependekeza iwe namna hiyo katika Katiba.

Ya tatu, ni hali ya vyama mingi. Siku hizi tuko na Kenya ya vyama vingi, ambavyo, chama ambacho kinatawala ama kilichokinga katika upande wa utawala, kinalalia wale watu ambao hawajakuwa, wakiwachagua. Kwa mfano, Maendeleo ikiwa pande hii, ni pande ya KANU, na pande ile ni pande ya chama ingine. Inakuwa tofauti kwa maendeleo. Hakuwezi kuwa na barabara, maendeleo haiwezi kuingia kwa sababu ni ya upinzani. Serikali iweke kiwango ya kwamba, wananchi ni watu wenye vyama vingi, na kila mahali ambao, chama kile kinashindwa, kisije kikaweza kushinda pamoja na wale watu. Wananchi wawe wakihudumiwa upande ya barabara, ma-hospitali na kila kitu. Hiyo iwe katika Katiba yetu, kwa sababu, tukishinda pande ya vyama vingi, inakuwa pengine, hata hakuna haja ya hospitali, hakuna kila kitu. Na dawa inakuwa taabu, kwa sababu wale ni watu wa upinzani.

(Interjection) Com. Muigai: Hilo jambo limesikika, neno la mwisho?

Daniel Kamotho: Jambo la mwisho ambalo ningetaka kusema, ni ya kwamba, katika mashamba yetu ambayo tuko nayo hapa, mimi ni mkulima, tunaambiwa tuangalie katika upande wa umaskini. Tuletewe maji, tuletewe barabara na tuletewe hospitali, ili tuweze kuendelea na kazi yetu katika mashamba yetu, kama vile sheria ilisema, miaka mia mbili, itakuwa kila mtu ako na sitima, maji, na barabara safi, na hiyo yote hatujapata katika Serikali tuliyo nayo. Sasa, Katiba ambayo itakuja, irekebishe hiyo. Asante.

Com. Muigai: Asante sana. Daniel Rugut? Na atafuatwa na Daniel Rotich, na James Kamau. Daniel Rugut.

Daniel Rugut: Kwa majina ni hayo, naitwa Evangelist Daniel Rugut, kutoka Rongai Constituency, Sumei Sub-location.

Ninatajia tu machache, kwa sababu mengi yametajwa, lakini ninaenda katika sehemu ya mashamba makubwa makubwa. Tunajua ya kwamba, kuna watu ambao wako na mashamba makubwa, na hawajawai kusitawisha hayo mashamba, na Serikali haipati chochote kutoka kwa hayo mashamba. Ningeonelea, inafaa, hawa watu wapewe high taxation, ili wafanyie hizo mashamba kazi, kwa sababu, Serikali inaombaomba vyakula, na tuko na mashamba makubwa ambayo ingeweza kutozelesha wananchi wa Kenya.

Ya pili, job opportunities should be guaranteed by the Government, one-man-one-job.

Area ingine ni kuhusu free education – masomo ya bure. At least from primary to secondary level, this can fight illiteracy in Kenya since we are very independent. In Kenya, we have not succeeded in these areas through the number of (inaudible), through the gap between the rich and the poor is rapidly increasing in a very high rate. Ningeonelea, kutoka primary mpaka secondary, lakini wale ambao wanajiunga na shule ya upili, wale genius, wanafunzi ambao wanaweza ku-acquire high points, na hawajiwezi, wapewe loans kama wale wanapewa katika vyi vikiu, ili waendeleo na masomo, kwa sababu, wengi wao wako na knowledge ya kuendelea na masomo, lakini, kuna poverty ambayo imetukabidhi sana wananchi wa Kenya, Serikali iangalie hawa, ili waendeleze masomo yao.

(Interjection) Com. Muigai: Una dakika nyingine moja.

Daniel Rugut: Ingingine moja, ni kuhusu Ministries in Kenya. Hiyo ni President, kwa election ya Cabinet Ministers. Tunaona ya kwamba, ma-Ministers wanakuwa eleted lakini haifuati kulingana na career zao. Tunaona ma-Ministers wengine, wanaweza kuchaguliwa, kwa mfano, Ministry of Health, na huyu Minister, career yake ni masomo ya agriculture. Ndio tunaona, ma-Ministries ina-collapse, kwa sababu, Ministers wengi wanaenda kusimamia Ministries ambazo hawajachukua kulingana na masomo yao. Kwa hivyo, ninaonelea ya kwamba, kama ni Ministries, Ministers wachaguliwe kulingana na career yao, kutokana na masomo yao, ili ma-Ministries zetu ziendeleo vizuri. Asanteni.

Com. Muigai: Asante. Daniel Rotich?

Daniel Rotich: Mimi ni Daniel Rotich. Ninataka kuongea mambo mawili tu, sina mambo mengi. Tunapendekeza Local Government, ambayo tunaona wanalipisha kodi kwa licencing, ningependekeza, waweke into classes. Town na interior reserve, iwe na pesa zao, ambapo town iwe bei ya juu kidogo, na reserve, iwe na bei ya chini.

Ya pili, mambo ya co-operative societies. Katika nchi hii yetu ya Kenya, sijui ni sheria imekosa, ili ilinde ile sheria, kwa sababu, ilinde ile co-operative, kwa sababu, unakuta Commissioners nyinyi, munakuta co-operative, wale watu wanapeleka maziwa katika ma-cooperative zao, unakuta mtu mmoja ama office-bearers wanaharibu, wanaharibu mambo ya cooperatives. Hakuna mahali ambapo wanaweza kushtakiwa. Unakuta mtu amekula pesa, na hakuna mahali tunaweza kushtaki yeye. Tukikata kumshtaki, hakuna sheria. So, tunaomba, nyinyi muweke mkaso, muweke sheria ambayo italinda cooperative societies. Ni hayo tu, sina maneno mengi. Nyingi imesemwa.

Com. Raiji: Asante. James Kamau? James Kamau? Julius Koskey? Julius Koskey? Stanley Soi – AIC? Hayuko. Jones Ng'eno. Utafuatwa....

Stanley Soi: Ninawakilisha memorandum ya AIC, Koitok, na nina machache ya kuzungumza, ambayo haiko katika memorandum hiyo.

Juu ya Katiba ya zamani, ninasema, free education, free health, na nilikuwa ninashughulika na juu ya kuondoa ujinga, na maradhi, na kuondoa umaskini. Ninapendekeza ya kwamba, Katiba mpya, irejeshwe jambo ilo, kwa sababu, tunajua, Serikali au Kenya, si maskini. Ina resources ya kutosha, ku-manage mambo hayo.

Ninapendekeza ya kwamba, mambo ya cost-sharing, isije kwa wana-Kenya tena, isiwe kwa wananchi tena.

Mambo ya natural resources. County councils ipewe jukumu ya kulinda natural resources ambazo ziko sehemu zao. Na faida ambayo inapatikana katika mambo hayo, wapewe percentage, kwa sababu hao ndio wenye kutunza natural resources hizo.

Mambo ya ma-shule pia. Tunasikia watoto wakipita waende secondary school, wanaambiwa, ili mpewe usaidizi, au bursaries, lazima wawe watoto werevu. Watoto wote wapewe bursaries. Kwa sababu tunaamini, wale wamepita na wako secondary schools, ni werevu, sio wajinga. Ni hayo tu ndio niko nayo. Asanteni.

Com. Raiji: Okay, jiandikishe hapo. John Langat? John Langat? Hayuko. Stephen Kimani? Okay, utafuatwa na Chepkonga Kiplenge.

Stephen Kimani: Asante sana Honourable Commissioners. Haya ni maoni yangu mimi binafsi, ambayo nilikuwa nina..... (inaudible), inafaa yatajwe hapa wakati ambapo munaokota maoni ya watu kuhusu Katiba mpya. Stephen Kimani ndilo jina langu.

